**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

# HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI - OFISI YA RAIS - KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA

**MHESHIMIWA MWL. HAROUN ALI SULEIMAN (MBM)**

**AKIWASILISHA KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025**

**MEI, 2024**

## YALIYOMO

**SEHEMU YA KWANZA** ........ 1
1.0 UTANGULIZI ........ 1
1.1. Salamu za Pongezi ........ 1
1.2. Mkono wa Pole ........ 3

**SEHEMU YA PILI** ........ 4
2.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 ........ 4
2.1. Ukusanyaji wa Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ........ 4
2.2. Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Mwaka 2023/2024 ........ 4
2.3. Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ........ 5
2.3.1. Fungu G01: Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora ........ 6
2.3.2. Fungu G02: Programu ya Usimamizi na Upatikanaji wa Haki ........ 17
2.3.3. Fungu G03: Programu ya Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Sheria ........ 19
2.3.4. Fungu G04: Programu ya Usimamizi wa Utekelezaji wa Kesi za Jinai ........ 20
2.3.5. Fungu G05: Programu ya Usimamizi wa Mapitio ya Sheria ........ 21
2.3.6. Fungu G12: Programu ya Uwezeshaji Wananchi Kishariah ........ 22
2.3.7. Fungu G13: Programu ya Huduma za Serikali Mtandao 24
2.3.8. Fungu G14: Programu ya Usimamizi na Uratibu wa Taasisi na Masuala ya Kiislamu ........ 25
2.3.9. Fungu G15: Programu ya Usimamizi wa Maadili ya Viongozi ........ 26
2.3.10. Fungu E04: Programu ya Ukaguzi na Udhibiti wa Fedha na Rasilimali za Umma ........ 27

2.3.11. Fungu E05: Programu ya Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi. .......... 27
2.3.12. Fungu E07: Programu ya Usimamizi wa Watumishi wa Umma .......... 28
2.3.13. Fungu E08: Programu ya Usimamizi wa Uajiri, Haki na Nidhamu kwa Watumishi Serikalini .......... 29

**SEHEMU YA TATU** .......... 31
3.0 MUELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 .......... 31
3.1. Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 .......... 31
3.2. Malengo Makuu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 .......... 31
3.3. Malengo ya Utekelezaji kwa Programu za Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 .......... 32
3.3.1Fungu G01: Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora (ORKSUUB) .......... 33
3.3.2 Fungu G02: Programu ya Usimamizi na Upatikanaji wa Haki- MAHAKAMA KUU .......... 39
3.3.3 Fungu G03: Programu ya Mageuzi ya Utoaji wa Huduma za Sheria- OFISI YA MWANASHERIA MKUU .......... 40
3.3.4 Fungu G04: Programu ya Usimamizi wa Utekelezaji wa Kesi za Jinai-OFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA.. 40
3.3.5 Fungu G12: Programu ya Haki na Uwezeshaji Kishariah-KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA.. 41
3.3.6 Fungu G13: Programu ya Huduma za Serikali Mtandao-MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO .......... 41
3.3.7 Fungu G14: Programu ya Usimamizi wa Masula ya Dini-OFISI YA MUFTI MKUU WA ZANZIBAR .......... 42
3.3.8 Fungu G15: Programu ya Usimamizi wa Maadili ya Viongozi-TUME YA MAADILI YA VIONGOZI .......... 43
3.3.9 Fungu E04: Programu ya Ukaguzi na Udhibiti wa Fedha

na Rasilimali za Umma-OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ................ 43
3.3.10 Fungu E05: Programu ya Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu Uchumi - ZAECA ...................... 44
3.3.11 Fungu E07: Programu ya Usimamizi wa Utumishi wa Umma ........................................................... 44
3.3.12 Fungu E08: Programu ya Usimamizi wa Uajiri, Haki na Nidhamu kwa Watumishi Serikalini ....................... 45

**SEHEMU YA NNE**.............................................................. 47
4.0 SHUKRANI NA HITIMISHO.............................................. 47
4.1 Shukrani ............................................................................ 47
4.2 Hitimisho............................................................................ 49
Kiambatisho Nam. 1a:........................................................... 50
Kiambatisho Nam. 1b: .......................................................... 51
Kiambatisho Nam. 1c:........................................................... 55
Kiambatisho Nam. 2: ............................................................ 56
Kiambatisho Nam. 3: ............................................................ 59
Kiambatisho Nam. 4 ............................................................. 59
Kiambatisho Nam. 5a:........................................................... 60
Kiambatisho Nam. 5b: .......................................................... 61
Kiambatisho Nam. 5c:........................................................... 63

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwa Baraza lako Tukufu lipokee, lijadili na kupitisha utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na kuidhinisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kwa Ofisi ya Rais-Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora.

2. **Mheshimiwa Spika**, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwingi wa Rehma, kwa kutuwezesha kukutana leo hii tukiwa na afya njema, na kutuwezesha kuendelea kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi tukiwa katika hali ya amani na utulivu.

### 1.1. Salamu za Pongezi

3. **Mheshimiwa Spika,** napenda kumpongeza kwa dhati Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi **Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi** kwa uongozi wake makini na umahiri mkubwa anaouonesha katika kuiongoza Zanzibar na kuiwezesha kupata mafanikio makubwa katika sekta zote za kiuchumi, kisiasa na kijamii. Aidha, tunampongeza kwa hatua kubwa aliyopiga katika kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020-2025 sambamba na kudumisha hali ya amani na utulivu pamoja na mshikamano wa wananchi wa Zanzibar.

4. **Mheshimiwa Spika,** nampongeza **Mheshimiwa Othman Masoud Othman,** Makamo wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar kwa anavyoshirikiana na Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa majukumu yake ya kuiongoza Zanzibar, kudumisha amani na kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar. Vilevile, nampongeza **Mheshimiwa Hemed**

**Suleiman Abdulla,** Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar, kwa kuendelea kuratibu na kusimamia shughuli za Serikali katika Baraza lako Tukufu na kumsaidia Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020/2025, pamoja na Mipango ya Maendeleo ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. Mafanikio tunayoyapata katika utekelezaji wa Ilani ni ya kupigiwa mfano. Bila ya shaka, kila mwananchi ni shahidi wa jambo hili.

5. **Mheshimiwa Spika,** naomba nikupongeze wewe binafsi na Naibu Spika kwa kuliongoza kwa umakini na umahiri Baraza hili Tukufu katika kufikia maamuzi mbalimbali yenye manufaa kwa maendeleo ya Zanzibar. Aidha, napenda kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati mbalimbali za Baraza la Wawakilishi kwa umahiri wao katika kusimamia utekelezaji na matumizi ya fedha za umma.

6. **Mheshimiwa Spika,** natoa shukurani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa chini ya Mwenyekiti wake **Mheshimiwa Machano Othman Said,** Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Mfenesini na Makamo Mwenyekiti **Mheshimiwa Maryam Thani** Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Gando kwa ushauri na miongozo waliyotupa katika utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024 na ushauri wao mzuri walioutoa wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Nalihakikishia Baraza lako Tukufu kwamba Wizara yangu itaendelea kuzingatia miongozo, maoni na ushauri wa Kamati.

7. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Makunduchi, kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kuwawakilisha katika Baraza lako Tukufu pamoja na katika kutekeleza kazi mbalimbali za maendeleo katika jimbo.

8. **Mheshimiwa Spika**, Naishukuru familia yangu hususan Mke wangu mpendwa na watoto wangu kwa mashirikiano yao wanayonipa katika utekelezaji wa majukumu yangu.

## 1.2. Mkono wa Pole

9. **Mheshimiwa Spika,** natoa pole kwa **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Watanzania wote, kwa kuondokewa na viongozi wetu wapendwa Hayati Alhaj Ali Hassan Mwinyi, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Pili na Hayati Edward Ngoyai Lowasa, Waziri Mkuu Mstaafu. Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi, Amina. Aidha, natoa pole pia kwa Rais wetu mpendwa **Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi** na familia yake kwa kuondokewa na mzee wao na tunamuomba Mwenyezi Mungu awape subra katika kipindi hiki kigumu.

10. **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo ya utangulizi, naomba sasa kuwasilisha taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Mpango wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**11.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara yangu imesimamia mafungu **13** ya Bajeti yaliyotekelezwa kupitia Programu kuu **16** ambazo zinatekelezwa na Idara na Taasisi zinazojitegemea zilizo chini ya Wizara. Utekelezaji wa Bajeti wa kila Programu inaelezwa kwa kina katika sehemu zinazofuatia za taarifa hii.

### 2.1. Ukusanyaji wa Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**12.** **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Ofisi ya Rais-Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kupitia Taasisi zilizo chini yake ilikadiriwa kukusanya mapato ya **Sh. 4,535,900,000** ukilinganisha na **Sh. 3,438,428,395** ilizokadiriwa mwaka 2022/2023, sawa na ongezeko la **Sh. 1,097,471,605** (asilimia 32 ya ongezeko).

**13.** **Mheshimiwa Spika,** hadi Machi 2024, **Sh. 2,033,471,629** zimekusanywa (asilimia 45 ya makadirio). Makusanyo haya yanatokana na vyanzo mbalimbali kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Nam. 1a.**

### 2.2. Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**14.** **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais-Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, ilipangiwa kutumia jumla ya **Sh. 80,584,431,552** ambapo kati ya hizo, **Sh. 51,241,200,000** ni kwa matumizi ya kazi za kawaida, mishahara na ruzuku na **Sh. 28,000,000,000**

zilipangwa kutumika kutoka katika Bajeti ya Maendeleo kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ya Ujenzi wa Mahkama za Mikoa na Wilaya, utayarishaji wa Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Taarifa za Kesi na Utekelezaji wa Programu ya Mageuzi ya Sheria na Utumishi wa Umma. Aidha, Wizara pia ilipangiwa kutumia Sh. 1,343,231,552 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

15. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2024, **Sh. 46,112,099,030** zimepatikana (57% ya lengo). Kati ya fedha zilizopatikana, **Sh. 36,821,376,149** (72% ya lengo) zilitumika kwa matumizi ya kazi za kawaida, mishahara na ruzuku na **Sh. 9,290,722,881** (33% ya lengo) zilitumika katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Programu ya Mageuzi ya Sheria na Utumishi wa Umma na Ujenzi wa Mahkama za Mikoa na Wilaya. Kwa upande wa Miradi inayofadhiliwa na Washirika wa Mendeleo, **Sh. 716,898,350** (53% ya lengo) zimepatikana **(Kiambatisho Nam. 1b & 1c).**

## 2.3. Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

16. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Ofisi ya Rais-Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora ilitekeleza Mpango na Bajeti kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo:
    (i) Kutekeleza Mpango wa Mabadiliko katika Sekta ya Sheria Awamu ya Pili;
    (ii) Kuendelea na Utekelezaji wa Mpango wa Mageuzi ya Utumishi wa Umma Awamu ya Pili;
    (iii) Kushughulikia Maslahi ya Watumishi wa Umma, Miongozo na Matoleo ya Kiutumishi pamoja na Miundo ya Kiutumishi ya Taasisi;
    (iv) Kuendeleza matumizi wa Mifumo ya Kieletroniki katika utumishi wa Umma;

(v) Kutayarisha na kutoa miongozo ya Utoaji wa Msaada wa Kisheria na kuandaa Mpango Kazi wa Kitaifa (NPA);
(vi) Kuongeza wigo wa upatikanaji wa msaada wa kisheria kwa wananchi waliowengi na walio katika mazingira duni;
(vii) Kuendelea kuimarisha utendaji katika taasisi za Sheria na kufanya marekebisho ya sheria mbalimbali;
(viii) Kuunganisha Mfumo wa Malipo na Mfumo wa Utumishi awamu ya pili katika Taasisi na Mashirika;
(ix) Kuendelea kuimarisha umoja na mshikamano pamoja na kudumisha Amani na Utulivu kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali;
(x) Kusimamia maadili katika utumishi wa umma na misingi ya utawala bora;
(xi) Kuongeza kasi katika mapambano dhidi ya vitendo vya rushwa na ubadhirifu wa mali ya umma; na
(xii) Kuongeza kasi katika Ukaguzi na Udhibiti wa Rasilimali za Umma.

17. **Mheshimiwa Spika,** Taarifa za utekelezaji, wa Bajeti na matumizi halisi kwa kila fungu na Programu zilizomo katika Ofisi ya Rais, ni kama ifuatavyo:-

### *2.3.1. Fungu G01: Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora*

18. **Mheshimiwa Spika,** Fungu G01 linahusisha Programu nne ambazo ni.

#### *(i) Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Sheria*

19. **Mheshimiwa Spika,** Programu inatekelezwa na Idara ya Katiba na Msaada wa Kisheria. Kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024, kazi zifuatazo zilitekelezwa: -

i Mkutano wa nusu mwaka wa kuratibu huduma za kutoa msaada kisheria umefanyika kwa lengo la

kujenga uelewa wa huduma zinatolewa ikiwa ni juhudi za Serikali katika kutoa huduma hizo. Washiriki 70 walihudhuria (wanawake 31 na wanaume 39);

ii Sera ya Msaada wa Kisheria ya Mwaka 2017 imefanyiwa mapitio na rasimu ya awali imekamilika;

iii Elimu kuhusiana na huduma za msaada wa kisheria, na upatikanaji wa haki imetolewa kupitia Jukwaa la Tatu la Msaada wa kisheria na vipindi vya redio na TV. Vipindi 16 vya redio na TV vimerushwa; na

iv Mikutano iliyolenga kujenga uwelewa kwa jamii kuhusu masuala ya udhalilishaji. imefanyika Unguja na Pemba na washiriki 65 walihudhuria (wanawake 40 na wanaume 25).

**20.** **Mheshimiwa Spika,** Mwaka wa Fedha 2023/2024 Programu ilipangiwa **Sh. 222,333,200** (mishahara Sh. 108,333,200 na matumizi mengineyo **Sh. 115,000,000).** Hadi kufikia Machi 2024, **Sh. 158,387,245** (71% ya lengo) zimepatikana ambapo Sh. 108,976,115 zilitumika kwa mishahara (101% ya lengo) na **Sh. 49,411,130** (43% ya lengo) zilitumika kwa matumizi mengineyo. Aidha, Idara ilipata **Sh. 42,130,000** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kupitia Mradi wa Kuimarisha Upatikanaji wa Haki Zanzibar (**Kiambatisho Nam. 1b).**

### *(ii) Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora*

**21.** **Mheshimiwa Spika,** Programu inatekelezwa na Idara ya Utawala Bora na utekelezaji kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ni kama ifuatavyo:-

i Elimu juu ya masuala ya utawala imetolewa katika mabaraza ya vijana, tasisi za Serikali na kwa wananchi kupitia vyombo vya habari. Vipindi 53 vya radio (Unguja 39 na Pemba 14) vimetayarishwa;

ii Mafunzo kwa umma juu ya masuala ya utawala bora yametolewa kupitia maonesho mbalimbali ikiwemo: Maonesho ya kuadhimisha Miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar ya 1964; Maonesho ya Siku ya Chakula Duniani Chamanangwe Pemba; Maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu pamoja Maadhimisho ya Siku ya Kuzuia Rushwa Barani Afrika; na

iii Tathmini juu ya Hali ya Upatikanaji wa Vyeti vya Kuzaliwa imefanyika na matokeo yameonesha kuimarika kwa hali ya upatikanaji wa huduma hizo.

**22.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Programu ilipangiwa **Sh. 316,566,320** (mishahara 216,566,320 na **Sh. 100,000,000** matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi 2024, **Sh. 153,668,000** zimepatikana (49% ya lengo) ambapo **Sh. 111,455,215** (51% ya lengo) zilitumika kwa mishahara na **Sh. 42,212,785** (42% ya lengo) zilitumika kwa matumzi mengineyo **(Kiambatisho Nam. 1b).**

### *(iii) Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora*

**23.** **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Idara ya Utumishi na Uendeshaji na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Kwa upande wa Idara ya Utumishi na Uendeshaji kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Idara imeendelea kusimamia uendeshaji wa Ofisi kwa kuhakikisha upatikanaji wa vitendea kazi, ukarabati mdogo wa Ofisi, usimamizi wa mali za umma na mafunzo kwa watumishi. Wafanyakazi wanane wanaoendelea na masomo ya muda mrefu katika fani za Sheria, Usimamizi wa Mifumo, Uhazili, na Usimamizi wa Rasilimali Watu wamepatiwa stahiki zao;

**24.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Idara ilipangiwa kutumia **Sh. 2,745,301,480** (mishahara **Sh. 1,645,301,480** na matumizi mengineyo **Sh. 1,100,000,000**). Hadi kufikia Machi 2024, **Sh. 2,285,024,716** (83% ya lengo) zilipatikana ambapo **Sh. 1,542,536,939** (94 ya lengo) zilitumika kwa mishahara na **Sh. 742,487,777** (67% ya lengo) zilitumika kwa uendeshaji wa Ofisi **(Kiambatanisho nam. 1b).**

**25.** **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, utekelezaji kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ni kama ifuatavyo:-

i Sheria ya Kamati za Uongozi imefanyiwa mapitio na Rasimu ya Mswada upo tayari na inatarajiwa kuwasilishwa katika Kamati ya Makatibu Wakuu;

ii Idara imekamilisha matayarisho ya Mpango Mkakati wa Wizara wa miaka mitano (2024/2028) na imesimamia mapitio ya Sera ya Utawala Bora, na Sera ya Msaada wa Kisheria. Rasimu za Awali zimekamilika;

iii Kikao kimoja cha mashirikiano baina ya Wizara ya Katiba na Sheria ya SMT na Ofisi ya Rais-Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kimefanyika. Kikao hiki kimeainisha maeneo ya mashirikiano kwa Taasisi za pande zote mbili zenye majukumu yanayofanana;

iv Idara kwa kushirikiana na shirika la UNDP imekamilisha matayarisho ya Mpango wa Kujenga Umahiri wa Watumishi wa Umma (Competency Framework for Public Service). Mpango huu unatarajiwa kusaidia katika kutayarisha mafunzo yanayohitajika kujenga umahiri wa Watumishi wa Umma-Zanzibar;

v Idara imesimamia na kuratibu majadiliano yalipelekea kutiliana saini baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia OR-KSUUB na Ubalozi wa Uingereza, Umoja wa Ulaya pamoja na Ubalozi wa Uswizi kwa ajili ya kuanzishwa Mradi wa Kujenga Mfumo

Endelevu wa Kupambana na Rushwa Tanzania-Zainzibar (BSAAT-Z). Mradi huu unalenga kujenga uwezo katika kupambana na uhalifu mkubwa wa kupangwa, rushwa, madawa ya kulevya, utakatishaji fedha haramu na silaha za maangamizi.

**26.** **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Idara ilipangiwa **Sh. 339,462,960** (**Sh. 189,462,960** mishahara na **Sh. 150,000,000** matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi 2024, **Sh. 45,343,267** (72% ya lengo), zimepatikana ambapo **Sh. 170,356,953** (90% ya lengo) ni mishahara na **Sh. 75,026,314** (50% ya lengo) ni matumizi mengineyo **(Kiambatisho Nam. 1b).**

## UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

**27.** **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kwa kushirikiana na Taasisi zilizopo chini ya Wizara, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2004 imeratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi mitatu ya maendeleo na kazi zilizotekelezwa ni kama ifuatavyo:

### *a) Mradi wa Uwezeshaji na Upatikanaji wa Haki Kisheria Awamu ya Pili (LEAP II)*

**28.** **Mheshimiwa Spika,** Mradi unatekelezwa kupitia Skuli ya Sheria, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Tume ya Kurekebisha Sheria, Chuo Cha Mafunzo na Idara ya Katiba na Msaada wa Kisheria na umejikita katika kusaidia kujenga uwezo wa Sekta ya Sheria na upatikajani wa haki kwa wananchi. Mradi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ulitumia **Sh. 508,105,500** na kazi zilizotekelezwa ni:-

i Skuli ya Sheria imeandaa Vitabu vya Muongozo vya Wakufunzi wa Skuli na Muongozo umeanza kutumika;
ii Ofisi ya Mwanasheria Mkuu imeandaa Kongamano la

Mawakili wa Serikali pamoja na Maafisa Sheria Zanzibar kujadili mafanikio na changamoto zinazoikabili Sekta ya Sheria;

iii Tume ya Kurekebisha Sheria imeandaa Ripoti ya Mapitio ya Sheria ya Msaada wa Kisheria, Sheria ya Adhabu na Sheria ya Makosa ya Jinai na ripoti zimewasilishwa kwa Taasisi husika na mapendekezo ya ripoti yameanza kufanyiwa kazi;

iv Chuo Cha Mafunzo kimetayarisha Muongozo wa Mafunzo kwa Wanafunzi waliokuwepo Vizuizini. Utekelezaji wa Muongozo huu umeanza;

v Idara ya Katiba na Msaada wa Kisheria imeendesha mafunzo kwa Wasaidizi wa Sheria Unguja na Pemba kwa lengo la kuwezesha kutoa huduma za msaada wa kisheria kwa ufanisi na wakati.

***b) Mradi wa Utoaji wa haki kwa Kuzingatia Jinsia ili kuwasaidia Wanawake Kukabiliana na Kesi za Ukatili Zanzibar***

**29.** **Mheshimiwa Spika,** Mradi unatekelezwa na Mahkama Kuu, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Tume ya Kurekebisha Sheria na Idara ya Katiba na Msaada wa Kisheria. Mradi umejikita katika kujenga uwezo wa wanawake katika kukabiliana na kesi za ukatili wa kijinsia. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 **Sh. 235,081,451** zilitumika na kazi zilizotekelezwa ni:-

i Mafunzo kwa Wasaidizi wa Sheria yalitolewa sambamba na mikutano ya vikundi mbalimbali vya kijamii ilifanyika Unguja na Pemba kwa lengo la kuwezesha upatikanaji wa huduma za msaada wa kisheria kwa jamii za mjini na vijijini;

ii Miongozo ya usimamizi na uendeshaji wa kesi imetayarishwa na kazi bado inaendelea;

iii Jukwaa la Jamii linalohusu masuala ya kijinsia

na kuripoti kesi za udhalilishaji na ukusanyaji wa takwimu limefanyika Unguja na Pemba. Washiriki 130 walihudhuria (wanawake 80 na wanaume 50).

***c) Mradi wa Kujenga Mfumo Endelevu wa Kupambana na Rushwa Tanzania (BSAAT).***

**30.** **Mheshimiwa Spika,** mradi huu ni wa miezi 15 na fedha zilizotengwa ni Pauni **1,500,000** na utekelezaji wake unazihusisha Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, ZAECA, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, kazi zilizofanyika ni kukamilisha taratibu za kuanza kazi Mradi na watendaji watano wameajiriwa, pamoja na ununuzi wa vitendea kazi.

**31.** **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Ofisi Kuu Pemba na kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024, kazi zifuatazo zilitekelezwa:-

i Ofisi ilisimamia uratibu wa majukumu ya Wizara kwa upande wa Pemba ambapo mikutano na ziara za kutembelea Wizara 15 pamoja na Taasisi 17 za Serikali zilifanyika la lengo la kuhimiza na kuelekeza utekelezaji wa miongozo ya Serikali inayohusu masuala ya kiutumishi;

ii Kuratibu na kufanya vikao viwili (2) vya watumishi (Matarishi 40 na Mafisa Utumishi 45) wa Wizara na Taasisi za SMZ kwa lengo la kusikiliza matatizo yanayowakabili na kuwapatia miongozo na maelekezo kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Kiutumishi.

**32.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Programu imepangiwa kutumia **Sh. 510,024,020** kwa mishahara na matumizi mengine. Hadi kufikia Machi 2024, **Sh. 326,567,480** (64% ya lengo) zimepatikana (mishahara

**Sh. 250,567,480** (75% ya lengo) na matumizi mengineyo **Sh. 76,000,000** (44% ya lengo) **(Kiambatanisho nam. 1b).**

***(v) Programu ya Usimamizi na Uendelezaji wa Watumishi wa Umma***

**33. Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa na Idara ya Mipango Rasilimali Watu na Maendeleo ya Watumishi na Idara ya Miundo ya Taasisi na Maslahi ya Watumishi. Kwa upande wa Idara ya Mipango Rasilimali Watu na Maendeleo ya Watumishi utekelezaji kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ulikuwa kama ifuatavyo: -

- i Idara imeratibu utayarishaji wa Mpango wa Miaka Mitano (5) wa Rasilimali Watu kwa Wizara na Taasisi zote za Umma;
- ii Uratibu wa fursa za mafunzo ya muda mrefu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo umefanyika na Watumishi 32 wamepata ufadhili wa masomo kwa ngazi ya Uzamili, watumishi 6 masomo ya ngazi ya uzamivu, na watumishi 26 mafunzo ya muda mfupi;
- iii Mafunzo juu ya matumizi ya Mfumo wa taarifa za Rasilimali Watu na Malipo yametolewa kwa Wizara na Taasisi zote ziliomo kwenye mfumo wa malipo ya Serikali. Aidha taarifa za watumishi wote zimeshafanyiwa mapitio na kuwekwa katika mfumo;
- iv Ukaguzi wa matumizi sahihi ya rasilimali watu umefanyika katika Mabaraza ya Miji, Manispaa na Halmashauri zote za Unguja na Pemba na Watumishi wa Wizara ya Afya kwa lengo la kuhakikisha matumizi sahihi ya rasilimali watu;
- v Mfumo wa maombi ya Ajira (ZanAjira) umefanyiwa marekebisho na sasa ajira zote za Wizara na Taasisi za Serikali zinafanyika kupitia Mfumo huo. Aidha, vibali 3,625 vya ajira mpya na 29 vya kujaza nafasi tupu vimetolewa kwa Wizara na Taasisi mbalimbali za Umma. Ruhusa ya nafasi 223 za ajira za kutwa zimetolewa kwa Wizara ya Maji, Nishati na Madini;

vi Kanuni za Uhamisho kwa Watumishi wa Umma kwenda nje ya Utumishi wa Zanzibar zimetayarishwa zipo katika hatua ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali;

**34.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Programu kwa upande wa Idara ya Mipango Rasilimali Watu na Maendeleo ya Watumishi ilipangiwa kutumia **Sh. 635,667,400 (Sh. 335,667,400** mishahara na Sh. 300,000,000 matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi 2024, **Sh. 399,883,856** (62% ya lengo) zimepatikana ambapo **Sh. 322,194,008** (96% ya lengo) zimetumika kwa mishahara na **Sh. 77,689,848** (26% ya lengo) zimetumika kwa matumizi mengineyo **(Kiambatisho Nam. 1b).**

**35.** **Mheshimiwa Spika,** utekelezaji kwa upande wa Idara ya Miundo ya Taasisi na Maslahi ya Watumishi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ulikuwa kama ifuatavyo:-

i Mapitio ya Miundo ya Taasisi/Wizara zote imefanyiwa kwa mujibu wa Hati idhini ya Serikali. Lengo ilikuwa ni kuhakikisha Wizara zinapangwa kwa mujibu wa majukumu ya msingi ya wazara husika;

ii Matayarisho ya Mifumo ya Kupima Utendajikazi wa Watumishi na Taasisi za Umma (Public Employee Performance Management Information System-PEPMIS na Public Institution Performance Management Information System-PIPMIS) yameanza. Hadidu rejea zimetayarishwa na kazi ya kutayarisha mfumo inatarajiwa kuanza mwaka ujao wa fedha;

iii Muongozo wa utayarishaji wa Mkataba wa Utowaji wa Huduma kwa Wateja umefanyiwa mapitio na rasimu itawasilishwa katika Vikao vya majadiliano kabla ya kuanza kutekelezwa rasmi;

iv Uhakiki wa mishahara kwa Mamlaka, Mashirika na Taasisi 22 zinazojitegemea zilizo chini ya Wizara nne (4) umefanyika na kasoro ziliopo katika ulipaji

wa mshahara na posho na utekelezaji wa miundo ya utumishi zimerekebishwa;

v Tathmini ya majukumu ya Taasisi imefanyika na Taasisi 15 za Usimamizi zenye majukumu yenye kufanana zimeunganishwa na Kampuni moja imefutwa. Hatua hii imelenga kupunguza wingi wa Taasisi, kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wananchi na kupunguza gharama za uendeshaji;

vi Mapitio ya Miundo ya Utumishi (Scheme of Service) imefanyika kwa lengo la kuziingiza kada za utumishi zilizokosekana na kuweka sifa linganishi za kielimu katika kada hizo. Hatua hii imelenga kuondoa kasoro zinazowakabili waombaji wapya wa ajira kushindwa kufanya maombi kutokana na sifa za kielimu na taaluma zao kutokuwemo katika Miundo ya awali;

**36.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Programu kwa upande wa Idara ya Miundo ya Taasisi na Maslahi ya Watumishi imepangiwa kutumia **Sh. 713,044,620** (**Sh. 519,344,620** mishahara na **Sh. 193,700,000** matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi 2024, **Sh. 553,737,316** (77% ya lengo) zimepatikana ambapo **Sh. 452,565,169** (87% ya lengo) zimetumika kwa mishahara na **Sh. 101,172,147** (52% ya lengo) zimetumika kwa matumizi mengineyo **(Kiambatisho Nam. 1b).**

## TAASISI ZINAZOPOKEA RUZUKU

**37.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora imesimamia ruzuku ya mishahara na matumizi mengineyo ya Chuo cha Utawala wa Umma na Skuli ya Sheria. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Taasisi hizi zimetekeleza mambo yafuatayo:-

### *a) Chuo cha Utawala wa Umma (IPA)*

**38.** **Mheshimiwa Spika,** Chuo cha Utawala wa Umma kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kimetekeleza kazi zifuatazo:-

- i Mafunzo elekezi kwa Watumishi wapya 2,254 kutoka katika Wizara na Taasisi za Umma yamefanyika Unguja na Pemba;
- ii Watumishi 211 kutoka katika Wizara na Taasisi mbalimbali za Umma wamewapatia mafunzo ya muda mfupi ya kuimarisha utendaji kazi;
- iii Wastaafu watarajiwa 51 kutoka Taasisi mbalimbali za Umma wamepatiwa mafunzo;
- iv Chuo kwa kushirikiana na wahusika mbalimbali wamefanya tafiti kuhusiana na masuala ya utumishi wa umma;
- v Wanafunzi 1,494 (Watumishi wa Umma 423 na Wananchi wengine 1,071) wamesajiliwa kwa masomo ya ngazi ya Shahada, Astashahada na Shahada ya kwanza;
- vi Watumishi 42 wa IPA wamepatiwa fursa za masomo ya muda mrefu, kati ya hao, 3 shahada ya kwanza, 15 shahada ya uzamili na 24 ngazi ya uzamivu. Aidha, watumishi 55 wamepatiwa mafunzo mafupi katika fani mbalimbali;
- vii Matayarisho ya michoro na bajeti kwa ajili ya ujenzi wa Tawi la Chuo Pemba yameanza na ujenzi unatarajiwa kuanza katika mwaka ujao wa fedha.

**39.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Chuo kilipangiwa ruzuku ya **Sh. 2,386,900,000** kwa malipo ya mishahara. Hadi kufikia Machi 2024, **Sh. 1,979,777,839** (83% ya lengo) zimepatikana. Aidha, Chuo kilipangiwa kukusanya **Sh. 2,035,900,000** kutokana na malipo ya ada za wanafunzi na kimefanikiwa kukusanya **Sh. 1,439,564,558** (71% ya makadirio).

### *b) Skuli ya Sheria Zanzibar*

**40. Mheshimiwa Spika,** Skuli ya Sheria Zanzibar. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kilitekeleza kazi zifuatazo:-

- i Wanafunzi 34 kutoka Taasisi za Serikali na Sekta binafsi wamewapatia mafunzo ya vitendo (Field);
- ii Wanafunzi wapya 28 wamesajiliwa katika mwaka wa masomo 2024 na wanaendelea na masomo;
- iii Skuli imewezesha wanafunzi wake kufanya mitihani ya uandishi (WPE) na kujipima uwezo binafsi (ICA) ambapo jumla ya mitihani saba (7) ilifanywa;
- iv Mchakato wa kuandaa Kanuni za Mitihani umeanza. Kanuni hizi zitatoa muongozo kwa watunga mtihani, wasimamizi na wanafunzi wa Skuli ya Sheria.

**41. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Skuli ya Sheria ilipangiwa kutumia ruzuku ya **Sh. 370,600,000** kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi 2024, **Sh. 260,497,000** (70% ya lengo) zimepatikana. Aidha, Skuli ilikadiriwa kukusanya mapato ya **Sh. 379,000,000,** hadi kufikia Machi 2024, **Sh. 51,940,000** (14% ya makadirio) zimekusanywa.

### *2.3.2. Fungu G02: Programu ya Usimamizi na Upatikanaji wa Haki*

**42. Mheshimiwa Spika,** Program inatekelezwa na Mahkama Kuu-Zanzibar na kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kazi zifuatazo zimetekelezwa:-

- i Mashauri 2,318 (jinai 1,478 na madai 840) yamepokelewa, na mashauri 870 yametolewa uamuzi na mashauri 1,448 yanaendelea kufanyiwa kazi;
- ii Mashauri 205 yamefunguliwa katika Mahkama Maalum za dhalilishaji, na mashauri 142 (yametolewa uamuzi sawa na asilimia 69 ya mashauri yaliyofunguliwa).

iii Kwa upande wa Mahkama ya Kadhi mashauri 1,817 yamefunguliwa na tayari mashauri 1,119 (62%) yametolewa uamuzi na mashauri 698 yanaendelea kufanyiwa kazi;

iv Mashauri 73 ya Madawa ya kulevya yamefunguliwa na Mashauri 33 yametolewa maamuzi sawa na 45% na Mashauri 40 yanaendelea kufanyiwa kazi;

v Mashauri 45 yamefunguliwa katika Mahkama ya watoto na 31 yametolewa maamuzi (69%) na Mashauri 14 yanaendelea kufanyiwa kazi; **(Kiambatisho Nam.3)**

vi Mahkama imeratibu vikao 3 vya ushirikiano na wahusika wa haki jinai kwa lengo la kuharakisha mienendo ya kesi;

vii Maadhimisho ya wiki ya sheria yamefanyika tarehe 07/02/2024 Mgeni rasmi alikuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa, Dkt. Hussein Ali Mwinyi; na

viii Maandalizi ya utekelezaji wa Mradi wa Maboresho ya Mahkama ya Zanzibar (Zi–Jump) yamefanyika. Mradi ni mkopo kutoka Benki ya Dunia na unatarajiwa kuanza rasmi mwezi wa Julai, 2024.

**43.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Mahkama Kuu ilipangiwa kutumia **Sh. 11,230,500,000** (**Sh. 7,462,900,000** mishahara na **Sh. 3,767,600,000** matumizi mengineyo). Hadi Machi 2024, **Sh. 6,444,343,402** (57% ya lengo) zimepatikana ambapo **Sh. 4,990,241,014** (77% ya lengo) zilitumika kwa mishahara na **Sh. 1,454,102,388** (23% ya lengo) zilitumika kwa matumizi mengineyo.

**44.** **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Miradi ya Maendeleo, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Mahkama ilipangiwa bajeti ya **Sh. 25,000,000,000** kwa Mradi wa ujenzi wa Mahkama za Mkoa na Wilaya na **Sh. 2,000,000,000** kwa Mradi wa Mifumo ya Kielektroniki. Hadi kufikia Machi 2024, **Sh. 9,081,930,031** (36% ya lengo) zimepatika katika Mradi wa Ujenzi wa Mahkama. **(Kiambatanisho nam. 1b and 1c).**

**45.** **Mheshimiwa Spika,** Mahkama ya Kadhi, ilipangiwa kutumia ruzuku ya **Sh. 1,681,000,000** hadi kufikia Machi 2024, **Sh. 1,117,252,081** (66% ya lengo) zimepatikana ambapo **Sh. 979,633,081** (88% ya lengo) zilitumika kwa mishahara na **Sh. 137,619,000** (12% ya lengo) zilitumika kwa matumizi mengineyo.

**46.** **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa mapato, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Mahkama ilikadiriwa kukusanya **Sh. 1,576,000,000** hadi Machi 2024, **Sh. 341,047,498** (22% ya makadirio) zimekusanywa.

### *2.3.3. Fungu G03: Programu ya Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Sheria*

**47.** **Mheshimiwa Spika,** Programu inatekelezwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024, Ofisi imetekeleza shughuli zifuatazo: -

- i Miswada ya Sheria 10 na Kanuni 27 za Sheria tofauti zimetayarishwa kwa lengo la kuzifanya Sheria hizo ziweze kutekelezeka kwa ufanisi Zaidi;
- ii Matangazo ya Kisheria 64 yametayarishwa na yamewasilishwa Wakala wa Serikali wa Uchapaji kwa ajili ya kuchapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali;
- iii Mikataba 722 imetolea ushauri, kati ya hiyo, 483 ya ununuzi wa Bidhaa na Huduma, 122 Ujenzi, 97 Ushauri elekezi na 20 ya kodi. Aidha, Hati za Makubaliano (MoU) 170 zinazohusu Sekta mbalimbali zilisainiwa;
- iv Ofisi iliendelea kuiwakilisha Serikali kwenye mashauri ya Kesi za madai na kutoa ushauri wa kisheria kuhusiana na mashauri hayo, kesi 51 zimefunguliwa mahkamani.

**48.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Programu ilipangiwa kutumia **Sh. 3,368,200,000** (**Sh.**

**2,379,400,000** mishahara na **Sh. 988,800,000** matumizi mengineyo). Hadi Machi 2024, **Sh. 2,394,404,027** (71% ya lengo) zimepatikana ambapo **Sh. 1,928,682,507** (81% ya lengo) zimetumika kwa mishahara na **Sh. 465,721,520** (47% ya lengo) zimetumika kwa matumizi mengineyo **(Kiambatisho Nam. 1b).**

### *2.3.4.Fungu G04: Programu ya Usimamizi wa Utekelezaji wa kesi za jinai*

**49. Mheshimiwa Spika,** Programu inatekelezwa na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kazi zilizotekelezwa ni:-

- i Kesi 824 zimefunguliwa katika Mahkama mbalimbali Unguja na Pemba, ambapo kesi134 ni za udhalilishaji, 53 za madawa ya kulevya, 16 za kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu, 35 za mauwaji na 586 zinahusisha usalama barabarani, wizi wa mazao na mifugo, wizi wa kuaminiwa na makosa mengineyo;
- ii Majalada 23 yamepokelewa kutoka ZAECA kwa ajili ya kuyatolea uamuzi ambapo majalada 13 yanaendelea na upelelezi, majalada 6 yamepelekwa Mahkamani na majalada 5 yamefungwa kwa sababu mbalimbali;
- iii Ofisi kupitia Kituo cha Kupambana na Uhalifu wa Kiuchumi (ECC) kimeendelea kupitia majalada ya kesi kubwa, majalada sita yamepokelewa na kufanyiwa kazi;
- iv Kituo cha Kupambana na Uhalifu wa Kupangwa na Unaovuka Mipaka (SOC) kiliopo Kidimni kimezinduliwa rasmi. Wajumbe 27 wa kikosi kazi, wamepatiwa mafunzo. Kituo kimepatiwa gari 9 kwa lengo la kurahisisha utekelezaji wa shughuli zake;
- v Madawati ya kutoa msaada kwa mashahidi na waathirika wa makosa ya jinai yameanzishwa katika Mahkama za Mikoa yote ya Unguja. Lengo kuanzishwa

kwa madawati hayo ni kuwasaidia na kuwaongoza mashahidi kufika katika Mahkama husika pamoja na kuwapa maelekezo muhimu kuhusiana na kesi zao;

vi Progamu ya kuwatembelea waathirika na wahanga wa makosa ya udhalilishaji Unguja na Pemba imeanzishwa na Waathirika 21 walitembelewa;

vii Watendaji 25 wamewapatia mafunzo kuhusu kuwahudumia mashahidi na waathirika;

viii Kituo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti Zanzibar kimedahili wanafunzi wapya 110 kwa mwaka wa masomo 2024 (65 Cheti na 45 Diploma);

ix Ofisi kupitia Kituo cha Sheria imekamilisha taratibu za utafiti kuhusiana na adhabu zinazotolewa kwa watoto katika kesi za udhalilishaji. Matokeo ya utafiti yatatumika kuishauri Serikali.

**50.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Programu hii ilipangiwa kutumia **Sh. 3,621,700,000** (mishahara **Sh. 2,621,300,000** na **Sh. 1,000,400,000** matumizi mengineyo) hadi Machi 2024 **Sh. 2,672,781,843** (73% ya lengo) zimepatikana ambapo **Sh. 2,248,125,843** (86% ya lengo) zimetumika kwa mishahara na **Sh. 378,656,000** (37% ya lengo) zimetumika kwa matumizi mengineyo. Aidha, ruzuku ya **Sh. 158,700,000** imepangwa kutumika kwa uendeshaji wa Kituo cha Sheria, ambapo hadi kufikia Machi 2024, ruzuku ya **Sh. 45,225,000** (28% ya lengo) zimepatikana **(Kiambatisho Nam. 1b).**

### *2.3.5. Fungu G05: Programu ya Usimamizi wa Mapitio ya Sheria*

**51.** **Mheshimiwa Spika,** Programu inatekelezwa na Tume ya Kurekebisha Sheria na kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kazi zifuatazo zimetekelezwa:-

i Ripoti za Sheria 12 za Sekta mbalimbali zimepitiwa na kutathmini mapungufu yake na kutoa mapendekezo

katika utekelezaji wake **(Kiambatisho Nam 4 kinahusika);**

ii Tume inaendelea kuandaa vitabu vidogo vidogo vinavyotoa tafsiri ya Sheria kwa lugha rahisi inayofahamika kwa wananchi kwa lengo la kuwaongezea ufahamu na kujua maana halisi ya kilichokusudiwa ndani ya Sheria hizo;

iii Elimu inayohusiana na athari za Madawa ya Kulevya imetolewa katika Skuli mbalimbali za Sekondari katika Mkoa wa Mjini;

iv Nakala 1,000 za toleo maalum la jarida lenye maudhui ya utakatishaji wa fedha haramu na mapato yatokanayo na uhalifu. Aidha, nakala 3,000 za jarida la 6 la Tume lenye maudhui ya ujasiriamali na uwezeshaji wananchi kiuchumi zimechapishwa na kusambazwa katika taasisi za Serikali na binafsi; na

v Elimu ya Sheria imeendelea kutolewa kupitia kipindi cha ZANZIBAR NA SHERIA kinachorushwa na Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) kila siku ya Jumatatu kuanzia saa 3:30 hadi 4:15 usiku.

**52.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Programu ilipangiwa kutumia **Sh.1,886,700,000** (mishahara **Sh. 827,400,000** na matumizi mengineyo Sh. 1,039,300,000). Hadi Machi 2024, **Sh. 963,857,217** (51% ya lengo) zimepatikana ambapo **Sh. 628,951,598** (65% ya lengo) zimetumika kwa mishahara na **Sh. 334,905,619** (35% ya lengo) zimetumika kwa matumizi mengineyo **(Kiambatisho Nam. 1b).**

### *2.3.6. Fungu G12: Programu ya Uwezeshaji Wananchi Kishariah*

**53.** **Mheshimiwa Spika,** Programu inatekelezwa na Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, kazi zifuatazo zimetekelezwa:-

i Tirka 1,293 imefungulia (Unguja tirka 1,050 Pemba tirka 243) kati ya hizo tirka 584 (Unguja 463, Pemba 121) warithi wamepewa haki zao. Aidha, majalada 3,977 yanaendelea kufanyiwa kazi;

ii Kamisheni imesajili wakfu mpya 29, nyumba 320 na mashamba 11 na yanaendelea kusimamiwa na kutolewa manufaa kwa wanufaika kwa mujibu wa wasia. Nyumba 4 za wakfu zimefanyiwa ukarabati, jumla ya **Sh. 818,810,395** zimetumika;

iii Zakka na Misaada ya kheri yenye thamani ya **Sh. 2,914,906,000** (inayojumuisha pesa taslim, chakula, nguo na vifaa vya elimu) imekusanywa na kugaiwa kwa wananchi wa Unguja na Pemba;

iv Maandalizi ya Hijja ya mwaka 2024 yanaendelea na mahujaji 1,997 wanatarajiwa kusafirishwa na taasisi 15 za Zanzibar, sawa na asilimia 67 ya mahujaji wote wa Tanzania kwa mwaka 2024. Aidha, elimu ya Hijja na Mfuko wa Hijja imeendelea kutolewa;

v Semina na mafunzo elekezi yametolewa kwa Masheha 169 na vipindi 21 vya Redio na 7 vya TV vimerushwa kwa lengo la kuelimisha taratibu za Mirathi na utekelezaji wa kazi za Kamisheni; na

vi Mpango wa Mageuzi ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana umetayarishwa na utekelezaji wake umeanza. Mpango unalenga kuimarisha utendaji wa Kamisheni kuwa wa kisasa ikizingatiwa misingi ya kiislamu. Aidha, watendaji sita wa Kamisheni wameshiriki mafunzo ya uendeshaji na usimamizi wa shughuli za Kamisheni katika nchi za Oman na Malaysia.

**54.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Programu ilipangiwa kutumia **Sh. 1,930,100,000** (mishahara **1,347,600,000** na **Sh. 582,500,000** matumizi mengineyo). Hadi Machi 2024, **Sh. 1,307,016,770** (68 ya lengo) zimepatikana, kati ya fedha hizo, **Sh. 1,077,597,464** (80% ya lengo) zimetumika kwa mishahara na **Sh.**

**229,419,306** (39 ya lengo) zimetumika kwa matumizi mengineyo. Aidha, Kamisheni ilikadiriwa kukusanya mapato **Sh. 220,000,00,** hadi Mwezi Machi 2024 **Sh. 127,919,573** (58% ya lengo) zimekusanya. **(Kiambatisho 1a na 1b)**

### *2.3.7. Fungu G13: Programu ya Huduma za Serikali Mtandao*

**55.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kazi zifuatazo zimetekelezwa:-

i Ukaguzi na tathmini katika Taasisi mbalimbali za Serikali kuhusiana na masuala ya TEHAMA umefanyika;

ii Taasisi 4 zimeunganishwa katika mfumo wa ZanMalipo kwa lengo la kudhibiti ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Taasisi hizo ni Taasisi ya Kondominiamu, Mamlaka ya Usafiri wa Baharini (ZMA), Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar (ZHSF) na Wakala wa Serikali Uchapishaji;

iii Matayarisho ya Mfumo wa Bajeti na Matumizi ya Serikali (BAMAS) yamekamilika na Mfumo umeunganishwa na Mfumo wa Bajeti ili kuwa na mfumo mmoja wa Bajeti na Matumizi Serikalini;

iv Rasimu za miongozo minne (4) inayohusu matumizi ya TEHAMA zimetayarishwa na zitasambazwa kwa wahusika kwa matumizi; na

v Mafunzo ya matumizi ya Mfumo wa ZanVibali yametolewa kwa Wakuu wa Taasisi za Serikali, Maafisa Wadhamini, Waratibu wa Taasisi pamoja na Maafisa TEHAMA na Utumishi Unguja na Pemba. Aidha kazi ya kuunganisha Mfumo wa ZanVibali na Mfumo wa E-Vibali wa Tanzania Bara inaendelea ili kurahisisha uthibitishaji wa vibali katika Viwanja vya Ndege.

**56. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Mamlaka ilipangiwa kutumia **Sh. 3,208,600,000** (mishahara **1,249,700,000** na matumizi mengineyo **Sh. 1,958,900,000).** Hadi Machi 2024, **Sh. 1,647,950,589** (51% ya lengo) zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **Sh. 1,097,650,589** (88% ya lengo) zilitumika kwa mshahara na **Sh. 550,300,000** (28% ya lengo) zimetumika kwa matumizi mengineyo. **(Kiambatisho Nam. 1b).**

### *2.3.8. Fungu G14: Programu ya Usimamizi na Uratibu wa Taasisi na Masuala ya Kiislamu*

**57. Mheshimiwa Spika,** Programu inatekelezwa na Ofisi ya Mufti Mkuu, kazi zilifanyika kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ni kama ifuatavyo:-

i Ofisi imeendelea kutatua migogoro mbalimbali ya kijamii iliyowasilishwa katika Ofisi ya Mufti. Migogoro hiyo inahusiana na ndoa, talaka, malezi, utelekezaji wa watoto. Miongoni mwa migogoro iliyowasilishwa migogoro 474 ilihusu talaka na migogoro 9 ni ya kutelekeza mke na watoto;

ii Mafunzo ya ndoa yameendelea kutolewa Unguja na Pemba, na wananchi 724 wamehitimu mafunzo hayo (426 wanaume na 298 wanawake);

iii Ofisi imeendelea kutoa elimu na nasaha kwa wananchi, ambapo masuala 69 yanayohusu tohara, funga, ndoa, talaka yaliyoulizwa yamejibiwa;

iv Misikiti 87 na Madrasa 143 zimesajiliwa katika maeneo ya Unguja na Pemba; na

v Vikao 7 vimefanyika ikiwemo vikao vya Kamati ya Kitaifa ya kuthibitisha kuandama kwa Mwezi na kuratibu utekelezaji wa shughuli ya Mwaka Mpya wa Kiisilam (1445H) pamoja na sherehe za Maulid ya Mtume (S.A.W) na kufanya kikao 1 cha Baraza la Ulamaa.

**58.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar ilipangiwa kutumia **Sh. 1,930,100,000** (mishahara **Sh. 1,347,600,000** na matumizi mengineyo **Sh. 582,500,000**). Hadi Machi 2024, **Sh. 1,022,336,107** (53% ya lengo) zimepatikana. Kati ya fedha hizo, **Sh. 824,336,107** (61% ya lengo) zimetumika kwa mishahara na **Sh. 198,000,000** (34% ya lengo) zimetumika kwa matumizi mengineyo. **(Kiambatisho Nam. 1b).**

### *2.3.9. Fungu G15: Programu ya Usimamizi wa Maadili ya Viongozi*

**59.** **Mheshimiwa Spika,** Programu inatekelezwa na Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kazi zifuatazo zimetekelezwa: -

- i Fomu 2,685 za viongozi zimepokelewa na kusajiliwa (107% ya makadirio). Aidha, Tume imeendelea kuchukua hatua kwa viongozi waliochelewa kurejesha fomu hizo;
- ii Viongozi wa Umma 250 wamehakikiwa ni 125% ya lengo la Viongozi 200 waliopangwa kuhakikiwa katika Mwaka wa Fedha 2023/2024;
- iii Malalamiko manane ya ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi yamepokelewa na kufanyiwa kazi. Kati ya malalamiko hayo, malalamiko 6 uchunguzi wake unaendelea na malalamiko 2 yamekamilika na kupatiwa ufumbuzi; na
- iv Elimu kuhusiana na maadili imeendelea kutolewa kwa viongozi mbalimbali katika Taasisi za Serikali.

**60.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Tume ilipangiwa kutumia **Sh. 1,301,100,000** (mishahara **Sh. 640,800,000** na **Sh. 660,300,000** matumizi mengineyo). Hadi Machi 2024, **Sh. 1,061,905,186** (82% ya lengo). Kati ya fedha hizo, **Sh. 710,191,936** (111% ya lengo) zimetumika kwa mishahara na **Sh. 351,713,250** (53% ya

lengo) zimetumika kwa matumizi mengineyo **(Kiambatisho Nam. 1b).**

### *2.3.10. Fungu E04: Programu ya Ukaguzi na Udhibiti wa Fedha na Rasilimali za Umma*

**61.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Ofisi imetekeleza kazi zifuatazo:-

- i Ofisi imefanya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali za Wizara, Idara na Taasisi za Umma kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kwa lengo la kuimarisha uwajibikaji, ukusanyaji wa mapato pamoja na matumizi bora ya rasilimali za Umma; na
- ii Ofisi imewapatia mafunzo ya muda mrefu, mfupi na mafunzo ya ukaguzi watendaji 202.

**62.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Programu ilipangiwa kutumia **Sh. 6,292,400,000** (mishahara **Sh. 4,483,900,000** na matumizi mengineyo **Sh. 1,808,500,000**). Hadi Machi 2024, **Sh. 7,059,322,012** (112% ya lengo) zimepatikana. Kati ya fedha hizo, **Sh. 5,250,822,012** (118% ya lengo) zimepatikana kwa ajili ya mishahara na **Sh. 1,190,297,650** (66% ya lengo) zimepatikana kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, Ofisi ilikadiriwa kukusanya **Sh. 325,000,000.** Hadi Machi 2024, **Sh. 73,000,000** (22% ya lengo) zimekusanywa **(Kiambatisho Nam. 1a na 1b).**

### *2.3.11. Fungu E05: Programu ya Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi.*

**63.** **Mheshimiwa Spika,** Programu inatekelezwa na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kazi zifuatazo zimetekelezwa:-

- i Tuhuma 445 za rushwa na uhujumu uchumi zimepokelewa, kati ya hizo tuhuma 290 zinaendelea na uchunguzi, tuhuma 39 zimefungwa na zimefanyiwa udhibiti, tuhuma 13 zimehamishiwa taasisi nyengine, tuhuma 90 zimetolewa ushauri na majalada 20 yamewasilishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kwa hatua za kisheria. Aidha, majalada sita yamefikishwa Mahkamani na kesi 2 zimetolewa hukumu;
- ii Mamlaka imeokoa **Sh. 2,502,850,373,** kati ya fedha hizo, **Sh. 2,351,597,623** zilirudishwa Serikalini na **Sh. 151,252,750** zilirudishwa kwa wananchi; na
- iii Mamlaka imefuatilia utekelezaji wa miradi yenye thamani ya **Sh. 573,830,801,712** katika Sekta mbalimbali na thamani halisi ya fedha za miradi hiyo imefanyika.

**64.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Programu ilipangiwa kutumia **Sh. 4,294,600,000** (mishahara **3,136,200,000** na matumizi mengineyo **Sh. 1,158,400,000).** Hadi Machi 2024, **Sh. 3,927,173,000** (91% ya lengo) zimepatikana. Kati ya fedha zilopatikana, **Sh. 3,302,835,175** (105% ya lengo) zimetumika kwa mishahara na **Sh. 625,000,000** (54% ya lengo) zimetumika kwa matumizi mengineyo **(Kiambatisho Nam. 1b).**

### *2.3.12. Fungu E07: Programu ya Usimamizi wa Watumishi wa Umma*

**65.** **Mheshimiwa Spika,** Programu inatekelezwa na Kamisheni ya Utumishi wa Umma. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Kamisheni imetekeleza kazi zifuatazo:-

- i Kamisheni imefanyia kazi na kuridhia Miundo 11 ya Taasisi na Miundo 5 ya Utumishi;
- ii Ukaguzi Maalum umefanyika kutathmini utekelezaji wa Mpango wa Urithishaji Uongozi na uwepo wa Fani Adimu kwa Wizara 8 za SMZ na Taasisi 16;

iii Ripoti ya Mwaka ya Hali ya Utumishi wa Umma kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 na Ripoti ya Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miundo ya Utumishi iliyoidhinishwa na Serikali zimetayarishwa na kuwasilishwa;

iv Ziara ya kiutendaji kutembelea Tume ya Utumishi wa Umma Tanzania Bara imefanyika kwa lengo la kubadilishana uzoefu katika ukusanyaji na uchambuzi wa Taarifa za Kiutumishi kwa kutumia mifumo ya kieletroniki;

v Elimu kwa jamii imetolewa kupitia vyombo vya habari kuhusu masuala ya utumishi pamoja na mujukumu ya Kamisheni.

**66.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kamisheni ilipangiwa kutumia **Sh. 1,249,800,000** mishahara **Sh. 728,000,000** na matumizi mengineyo **520,900,000.** Hadi Machi, 2024, **Sh. 883,954,249** (71% ya lengo) zimepatikana. Kati ya fedha hizo, **713,562,249** (98% ya lengo) zimetumika kwa mishahara na **Sh. 170,392,000** (33 ya lengo) zimetumika kwa matumizi mengineyo **(Kiambatisho Nam. 1b).**

### *2.3.13.Fungu E08: Programu ya Usimamizi wa Uajiri, Haki na Nidhamu kwa Watumishi Serikalini*

**67.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa na Tume ya Utumishi Serikalini. Utekelezaji wa kazi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ni kama ifuatavyo: -

i Vibali vya ajira 957 vimetolewa kwa Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali Unguja na Pemba **(Kiambatisho Nam. 5a kinahusika);**

ii Watumishi 2,057 wamethibitishwa kazi, 280 wamepandishwa daraja na 330 wamebadilishwa kada watumishi. Aidha, Tume imeidhinisha kustaafu kwa hiari watumishi 12, imeridhia kuacha kazi kwa watumishi 5, imewastaafisha kazi kwa maradhi watumishi tisa 9 na Watumishi 557 wamestaafu kazi

kwa kufikia umri wa lazima; **(Kiambatisho Nam. 5b kinahusika);**

iii Watumishi 9 wameidhinisha kufukuzwa kazi baada ya kupatikana na makosa ya kinidhamu na watumishi 3 wameachishwa kazi baada ya kwenda kinyume na Sheria na Kanuni na Miongozo ya Utumishi wa Umma; (Kiambatisho Nam. 5c kinahusika); na

iv Mafunzo juu ya uelewa wa ajira na matumizi ya mfumo wa uombaji ajira (Zanajira) na kuepuka utoaji wa rushwa ili kupata ajira yametolewa kwa wanafunzi.

**68.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Programu imepangiwa kutumia **Sh. 867,700,000** (mishahara **458,600,000** na matumizi mengineyo **409,100,000**). Hadi Machi 2024, **Sh. 574,468,124** zimepatikana, (66% ya lengo). Kati ya fedha hizo, **Sh. 441,357,124** (96% ya lengo) zimetumika kwa mishahara na **Sh. 133,111,000** (33% ya lengo) zimetumika kwa matumizi mengineyo **(Kiambatisho Nam. 1b).**

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MUELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**69. Mheshimiwa Spika,** Bajeti ya Ofisi ya Rais-Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha wa 2024/2025, imezingatia Mpango Mkakati wa Wizara 2024/2029, Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021/2026, Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050, Sera za Wizara na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) 2020/2025.

### *3.1. Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025*

**70. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora imepanga kutekeleza bajeti kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo:-

i Kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Urithishaji Viongozi (Succession Plan);

ii Kuendeleza matumizi ya Mifumo ya Kielektroniki katika Utumishi wa Umma;

iii Kuendelea kuimarisha utendaji katika taasisi za Sheria na kufanya marekebisho ya Sheria mbalimbali;

iv Kuendelea kuongeza uwelewa kwa jamii juu ya masuala ya msaada wa kisheria; na

v Kusimamia misingi ya utawala bora, maadili na kuongeza mapambano dhidi ya Rushwa pamoja na ukaguzi na Udhibiti wa Rasilimali za Umma.

### *3.2. Malengo Makuu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025*

**71. Mheshimiwa Spika,** ili kufanikisha utekelezaji wa vipaumbele vya Ofisi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Ofisi ya Rais-Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

i Kuimarisha upatikanaji wa haki na utawala wa sheria;
ii Kusikiliza kesi na kutoa maamuzi ya haraka na kwa wakati;
iii Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Mafunzo ya Watumishi wa Umma kwa ajili ya upatikanaji wa Rasilimali Watu wenye sifa;
iv Kuimarisha matumizi ya mifumo ya kieletroniki katika shughuli na utoaji wa huduma za Serikali na kukuza uchumi;
v Kuimarisha misingi ya utawala bora, uwajibikaji na maadili katika utendaji wa shughuli za Serikali; na
vi Kuimarisha usimamizi wa udhibiti na rasilimali za Serikali.

### *3.3. Malengo ya Utekelezaji kwa Programu za Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025*

**72.** **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo haya sasa naomba kuwasilisha malengo ya utekelezaji kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kwa Programu za Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora.

**73.** **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 itatekeleza malengo yake kupitia mafungu ya bajeti 11 na Programu Kuu 15. Malengo ya utekelezaji kwa kila Fungu la Bajeti na Programu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ni kama inavyowasilishwa hapo chini.

**74.** **Mheshimiwa Spika,** kati ya Programu hizi, Programu kuu nne (4) za fungu G01 zinasimamiwa na kutekelezwa kupitia Idara zilizo chini ya Katibu Mkuu na Programu Kuu 11 zinatekelezwa na Taasisi zinazojitegemea.

### 3.3.1 *Fungu G01: Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora (ORKSUUB)*

**75.** **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais-Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma inasimamia Programu nne (4) na Taasisi mbili za ruzuku ambazo ni:-

***(i) Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Sheria***

**76.** **Mheshimiwa Spika,** kupitia utekelezaji wa Programu hii, Idara ya Katiba na Msaada wa Kisheria kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 imepanga kutekeleza yafuatayo: -

- i Kutekeleza Kampeni ya Kitaifa ya msaada wa kisheria ya Mama Samia kwa wananchi 1,600;
- ii Kuratibu, kuendesha na kusimamia utoaji msaada wa kisheria;
- iii Kusimamia vituo vya msaada wa kisheria na kufanya mikutano ya robo mwaka ya masuala ya msaada wa kisheria; na
- iv Kutoa elimu kwa jamii na kufanya mikutano ya masuala ya udhalilishaji na ushauri nasaha kwa wahusika wa udhalilishaji.

**77.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Idara imepangiwa kutumia **Sh. 322, 791,520** kwa matumizi ya kazi za kawaida. **(Kiambatisho Nam. 2).**

***(ii) Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora***

**78.** **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- i Kuijengea uwezo jamii kuhusu masuala mbalimbali ya utawala bora na haki za binadamu;
- ii Kuanzisha Sheria ya Usimamzi wa Utawala Bora; na
- iii Kuimarisha Uwajibikaji wa Watumishi na Taasisi za Umma na kufanya tathmini mbalimbali za Utawala Bora;

79. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha Idara kutekeleza Programu hii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, imepangiwa kutumika **Sh. 303,368,72**0 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. **(Kiambatisho Nam. 2).**

### *(iii) Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa ORKSUUB*

80. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina maeneo mawili ya utekelezaji eneo la uendeshaji ambalo linatekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi na eneo la uratibu linalotekelezwa na Mipango, Sera na Utafiti.

81. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Uendeshaji na Utumishi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, imepanga kutekeleza yafuatayo:-

- i Kutoa huduma za kiutumishi na stahiki za kiutumishi kwa wafanyakazi wa Ofisi;
- ii Kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu, mfupi na mafunzo kwa vitendo; na
- iii Kusimamia masuala ya uendeshaji wa Wizara na kuweka mazingira bora ya ufanyajikazi.

82. **Mheshimiwa Spika,** Idara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, imepangiwa kutumia **Sh. 3,388,050,096** kwa matumizi ya kazi za kawaida. **(Kiambatisho Nam. 2).**

83. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

- i Kuratibu mapitio na matayarisho ya Sera, Sheria, utekelezaji wa mipango ya bajeti;
- ii Kutayarisha Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini pamoja na Mpango wa Takwimu wa Wizara kwa lengo la kurahisisha ufuatiliaji na kupima kiwango cha ufanisi wa majukumu ya Wizara.

iii Kuratibu na kuandaa nyaraka za kisera na kisheria zitakazowasilishwa Serikalini;

iv Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Programu ya Mpango wa Mageuzi ya Sekta ya Sheria na Programu ya Mpango wa Mageuzi ya Utumishi wa Umma wa Awamu ya Pili.

v Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Miradi ya Wizara ikiwemo: (i) Mradi wa Mfumo Endelevu wa Kupambana na Rushwa Tanzania (BSAAT); (ii) Programu ya Utoaji wa Haki kwa Kuzingatia Jinsia na (iii) Programu ya Uwezeshaji wa Kisheria na Upatikanaji wa Haki Awamu ya Pili. Programu hizi zitatekelezwa kupitia ufadhili wa Mashirika ya Maendeleo ambao ni UNDP na UN-Women, Ubalozi wa Uingereza, Uswisi na Umoja wa Ulaya

**84.** **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha program hii kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, imepangiwa kutumia **Sh. 400,376,480** kwa matumizi ya kazi za kawaida. **(Kiambatisho Nam. 2).**

**85.** **Mheshimiwa Spika,** Ofisi Kuu Pemba itaendelea kuratibu na kusimamia shughuli zote za utawala na utumishi, mipango na bajeti zinazotekelezwa na Ofisi kwa upande wa Pemba. Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 imepangiwa kutumia **Sh. 625,072,800** kwa matumizi ya kazi za kawaida. **(Kiambatisho Nam. 2).**

## ***(iv) Programu ya Uendelezaji wa Watumishi wa Umma.***

**86.** **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Usimamizi na Uendelezaji wa Watumishi wa Umma inatekelezwa na Idara ya Mipango ya Rasilimali Watu na Maendeleo ya Watumishi pamoja Idara ya Miundo ya Taasisi, Utumishi na Maslahi ya Watumishi.

**87. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Usimamizi na Uendelezaji wa Watumishi wa Umma, Idara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i Kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Rasilimali Watu katika Utumishi wa Umma;

ii Kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Mafunzo ya Taasisi za Umma na upatikanaji wa mafunzo yanayotolewa na Washirika wa Maendeleo;

iii Kuandaa Mpango wa Mafunzo ya kujenfga umahiri wa Watumishi wa Umma

iv Kuzipatia mafunzo Taasisi za Umma juu ya matumizi ya Mfumo wa Rasilimali Watu na Malipo pamoja na Mfumo wa ZanAjira na kufuatilia utendajikazi wa Mifumo hiyo;

v Kuendelea kufanya uhakiki wa watumishi waliopo kuhakikisha kuna ufanisi katika matumizi ya rasilimali watu waliopo; na

vi Kuweka mazingira bora ya kazi na mahusiano mazuri baina ya Waajiri na Waajiriwa kupitia chombo cha Kitaifa cha majadiliano.

**88. Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha Programu hii kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 imepangiwa kutumia **Sh. 841,471,120** kwa matumizi ya kazi za kawaida. **(Kiambatisho Nam. 2).**

**89. Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa Programu hii kwa upande wa Idara ya Miundo ya Taasisi na Maslahi ya Watumishi, imepanga kutekeleza yafuatayo katika Mwaka wa Fedha 2024/2025:-

i Kufanya mapitio ya Miundo ya Taasisi kwa kuiwezesha kukidhi mahitaji ya kuwalenga wataka huduma;

ii Kukamilisha ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miundo ya Utumishi katika Taasisi za Umma;

iii Kusimamia uandaaji na utekelezaji wa Mifumo ya Kupima Utendajikazi wa Watumishi na Taasisi za

Umma (Public Employee Performance Management Information System-PEPMIS na Public Institution Performance Management Information System-PIPMIS);

iv Kukamilisha Utekelezaji wa Mkataba wa Utoaji wa huduma kwa Umma na tathmini ya Upimaji Utendaji Utumishi kwa Taasisi na Wizara za Serikali; na

v Kufanya uhakiki wa Mishahara pamoja na vyeti vya kumalizia masomo na Maposho kwa Watumishi.

**90.** **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha Idara kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 imepangiwa kutumia **Sh. 848,569,200** kwa matumizi ya kazi za kawaida. **(Kiambatisho Nam. 2).**

## TAASISI ZINAZOPOKEA RUZUKU

**91.** **Mheshimiwa Spika,** Ofisi Rais - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora inasimamia Taasisi mbili zinazopokea ruzuku ambazo ni Chuo cha Utawala wa Umma (IPA) na Skuli ya Sheria.

### *a) Chuo Cha Utawala wa Umma*

**92.** **Mheshimiwa Spika,** Chuo Cha Utawala wa Umma kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kimepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i Kuandaa na Kuendesha Programu za Mafunzo ya kuimarisha utendaji kazi kwa watumishi 1,000 kulingana na mahitaji yaliyopo katika Utumishi wa Umma;

ii Kuandaa na Kuendesha Programu za Mafunzo ya Awali kwa waajiriwa wapya 2,000 wa Serikali;

iii Kufanya Tafiti tatu (3) katika Utumishi wa Umma ili kubaini mapungufu yaliyopo katika Utumishi na kuandaa Programu za Mafunzo ya kujenga uwezo ili kuondooa mapungufu hayo; na

iv Kuandaa na Kuendesha Programu za Mafunzo ya Muda mrefu kwa Watumishi wa Umma 530 na wananchi wengine 2,065 kutokana na mahitaji ya kiutumishi katika ngazi ya Shahada, Stashahada na Astashahada.

**93.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Chuo kimepangiwa ruzuku ya **Sh. 3,191,000,000** kwa ajili ya mishahara. Aidha, Chuo kimepanga kukusanya **Sh. 3,243,805,000** kutokana na malipo ya ada za wanafunzi **(Kiambatisho Nam 2)**

### *b) Skuli ya Sheria Zanzibar*

**94.** **Mheshimiwa Spika,** Skuli ya Sheria Zanzibar kupitia Programu ya Mafunzo ya Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i Kutoa mafunzo ya vitendo kwa wahitimu wa fani ya sheria 50 kutoka Vyuo Vikuu katika ngazi ya Shahada ya kwanza;

ii Kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo wanasheria waliomo ndani na nje ya Serikali, waheshimiwa Majaji 14, Mahakimu 66 (wanawake 23 na wanaume 43), Makadhi 20, Mawakili 200, Wasaidizi wa Sheria pamoja na watoa Msaada wa Kisheria 400; na

iii Kufanya utafiti kuhusiana na masuala ya kisheria.

**95.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Skuli ya Sheria imepangiwa kutumia **Sh. 1,012,500,000** kwa ajili ya ruzuku ya matumizi ya kawaida. Aidha, Skuli imepanga kukusanya **Sh. 179,500,000** kupitia malipo ya ada za wanafunzi na uendeshaji wa mafunzo mafupi. **(Kiambatisho Nam. 2)**

### *3.3.2 Fungu G02: Programu ya Usimamizi na Upatikanaji wa Haki- MAHKAMA KUU*

**96. Mheshimiwa Spika,** Programu hii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i Kuimarisha upatikanaji wa Haki;

ii Kuharakisha huduma za Mahkama na Usimamizi wa Mashauri;

iii Kukuza imani na uelewa kwa jamii pamoja na hadhi ya Mahkama;

iv Kuendelea na matayarisho na kuanza matumizi ya Mifumo ya kieletroniki katika utowaji wa haki;

v Kukamilisha matayarisho na kuanza utekelezaji wa Mradi wa Kuimarisha Sekta ya Sheria (Zanzibar Judiciary Modernisation Programme – Zi-Jump); na

vi Kuimarisha usimamizi wa utendaji, uhamasishaji wa rasilimali na uhusiano wa kimkakati na washirika.

**97. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Programu imepangiwa kutumia **Sh. 68,900,700,000** kwa matumizi ya kazi za kawaida. Kati ya hizo, Mahkama Kuu imepangiwa kutumia jumla ya **Sh. 12,372,800,000.** Mahkama ya Kadhi imepangiwa kutumia **Sh. 1,964,700,000.** Kwa upande wa Bajeti ya Maendeleo, Mahkama imepangiwa kutumia **Sh. 54,500,000,0000** ambapo **Sh. 24,900,000,000** kwa Mradi wa ujenzi wa Mahkama za Mikoa na Wilaya, **Sh. 500,000,000** kwa Mradi wa Mfumo wa Kielektroniki wa Mahkama, **Sh. 600,000,000** ni mchango wa Serikali katika uendeshaji wa mradi wa Benki ya Dunia. Vilevile, Mahkama inatarajia kupata **Sh. 25,500,000,000** kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Zi – Jump na **Sh. 3,000,000,000** ni mchango kutoka Benki ya Dunia kupitia Mahkama ya Tanzania Bara.

**98. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Mahkama imepangiwa kukusanya mapato ya **Sh. 1,239,900,000. (Kiambatisho Nam. 1a & 2).**

### *3.3.3 Fungu G03: Programu ya Mageuzi ya Utoaji wa Huduma za Sheria- OFISI YA MWANASHERIA MKUU*

**99.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 imepanga kutekeleza yafuatayo: -

i Kuimarisha Mfumo wa Kielektroniki wa kutayarisha, kuhifadhi na kusimamia masuala yote yanayohusu uandishi wa sheria, kanuni na matangazo ya kisheria;

ii Kuendelea kusimamia na kutekeleza Mikataba ya Serikali 850 kikanda na kimataifa pamoja na kutoa ushauri wa kisheria katika Hati za Makubaliano (MoU);

iii Kuendelea kuiwakilisha Serikali Mahkamani dhidi ya Kesi zote za Madai, kufuatilia indhari za kuishtaki Serikali pamoja na kufanya Uchambuzi na Ushauri katika masuala mbalimbali ya Kesi za Madai; na

iv Kufanya Mapitio ya Sheria na kuzichapisha pamoja na kuwajengea uwezo wafanyakazi kwenye Uandishi wa Sheria, Usimamizi wa Kesi na masuala ya Mikataba.

**100.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Programu imepanga kutumia **Sh. 5,912,100,000** kwa matumizi ya kawaida. **(Kiambatisho Nam. 2).**

### *3.3.4 Fungu G04: Programu ya Usimamizi wa Utekelezaji wa Kesi za Jinai-OFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA*

**101.** **Mheshimiwa Spika,** Programu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 imepanga kutekeleza yafuatayo:-

i Kuimarisha miundombinu ya Ofisi kwa kujenga Ofisi mpya katika ngazi za mikoa na kukarabati zilizopo;

ii Kushirikiana na Taasisi mbalimbali za kitaifa, kikanda na kimataifa katika masuala ya haki jinai;

iii Kuwajengea uwezo waendesha mashtaka hasa katika eneo la mashtaka mahsusi (Specialization); na

iv Kuimarisha kitengo cha kulinda mashahidi na kusimamia kazi za kamati ya kuzuia udhalilishaji.

**102.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Programu imepangiwa kutumia **Sh. 5,636,600,000** kwa matumizi ya kawaida. Aidha ruzuku ya **Sh. 190,400,000** imepangwa kutumika kwa ajili ya Kituo cha Utafiti wa Sheria. Pia, Kituo kinatarajia kukusanya mapato ya **Sh. 334,060,000 (Kiambatisho Nam. 1a na 2).**

### *3.3.5 Fungu G12: Programu ya Haki na Uwezeshaji Kishariah-KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA*

**103.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i Kufanya mapitio ya Sheria ya Wakfu na Muundo wa Taasisi;

ii Kuendeleza Miradi na Uwekezaji wenye Tija;

iii Kuimarisha utendaji na huduma za Kamisheni kwa kuongeza matumizi ya TEHAMA katika kutoa huduma na uhifadhi wa kumbukumbu; na

iv Kuimarisha mazingira ya Ofisi na utoaji wa huduma.

**104.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Programu hii imepangiwa kutumia **Sh. 2,229,500,000** kwa matumizi ya kawaida. Kamisheni inatarajia kukusanya mapato ya **Sh. 272,777,000 (Kiambatisho Nam. 1a na 2).**

### *3.3.6 Fungu G13: Programu ya Huduma za Serikali Mtandao-MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO*

**105.** **Mheshimiwa Spika,** kazi zifuatazo zimepangwa kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2024/2025:

i Kuandaa kanuni za Sheria ya Mamlaka Serikali

Mtandao ya mwaka 2024 pamoja na kukamilisha Muundo wa Taasisi na Muundo wa Utumishi wa Mamlaka;

ii Kufanya mapitio ya Mpango Mkakati wa Mamlaka;

iii Kujenga uwezo wafanyakazi wa Wakala wa Serikali Mtandao katika utumiaji wa mifumo ya TEHAMA;

iv Itaimarisha Miundombinu ya Pamoja (shared infrastructure) ya Serikali Mtandao;

v Kuimarisha usalama wa mifumo pamoja na kuandaa miongozo mbalimbali; na

vi Kusimamia mifumo ya ukusanyaji wa mapato.

**106.** **Mheshimiwa Spika,** Programu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, imepangiwa kutumia **Sh. 3,695,800,000** kwa matumizi ya kawaida. **(Kiambatisho Nam. 2).**

### *3.3.7 Fungu G14: Programu ya Usimamizi wa Masula ya Dini-OFISI YA MUFTI MKUU WA ZANZIBAR*

**107.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kuimarisha utowaji wa fatwa, utafiti na usuluhishi wa migogoro;

ii. Kuimarisha uratibu na usimamizi wa mambo ya kiislamu na kuzijengea uwezo taasisi za kiislamu;

iii. Kuimarisha shughuli za kiislamu na kinga juu ya haki za wanawake na watoto; na

iv. Kuimarisha utendaji wa kazi za Ofisi.

**108.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Programu imepangiwa kutumia **Sh. 2,382,300,000** kwa kazi za kawaida na **Sh. 87,000,000** ruzuku kutoka kwa Wahisani **(Kiambatisho Nam. 2).**

### *3.3.8 Fungu G15: Programu ya Usimamizi wa Maadili ya Viongozi-TUME YA MAADILI YA VIONGOZI*

**109. Mheshimiwa Spika,** Programu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kupokea, kuhifadhi na kusajili pamoja na kuhakiki taarifa za mali na madeni ya viongozi wa umma 2,500;
ii. Kupokea malalamiko 20 na kufanya uchunguzi wa uvunjwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma;
iii. Kuelimisha Viongozi wa Umma na wananchi Unguja na Pemba kuhusu umuhimu wa kuzingatia Maadili;
iv. Kuendelea kuadhimisha kitaifa Siku ya Maadili na Haki za Binadamu; na
v. Kusikiliza na kutoa maamuzi kuhusu malalamiko na madai ya uvunjaji wa maadili ya viongozi wa umma;
vi. Kuwapatia mafunzo watumishi ili kuongeza umahiri.

**110. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Programu imepangiwa kutumia **Sh. 1,948,300,000** kwa matumizi ya kawaida **(Kiambatisho Nam. 2).**

### *3.3.9 Fungu E04: Programu ya Ukaguzi na Udhibiti wa Fedha na Rasilimali za Umma-OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI*

**111. Mheshimiwa Spika,** program hii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-
i. Ofisi itaendelea kufanya majukumu yake ya kikatiba ya kukagua mahesabu ya Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yakiwemo Mawizara, Mashirika na Taasisi mbalimbali pamoja na Miradi ya Maendeleo;
ii. Kudhibiti matumizi mabaya ya rasilimali za Serikali kwa manufaa ya wananchi wa Zanzibar; na
iii. Kuwajengea uwezo watendaji katika fani mbali ili kuimarisha kasi na ari na uwezo wa kutekeleza majukumu yao.

112. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Programu imepangiwa kutumia **Sh. 7,823,300,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Ofisi imepangiwa kukusanya mapato ya **Sh. 322,400,000. (Kiambatisho Nam. 1a na 2).**

### *3.3.10 Fungu E05: Programu ya Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu Uchumi*

113. **Mheshimiwa Spika,** program hii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

   i. Mamlaka itaelekeza nguvu zake katika Udhibiti wa vitendo vya rushwa katika ununuzi kwa Taasisi za umma, ukusanyaji wa mapato na matumizi ya Serikali pamoja na maeneo ya huduma za kijamii.
   ii. Itaendelea kufuatilia utekekelezaji wa miradi ya maendeleo, kufanya uchunguzi wa vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi.
   iii. Kutoa elimu kwa wananchi kupitia mikutano 276 na vipindi vya redio na televisheni 12 juu ya vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi ili kuhakikisha fedha za Serikali zinatumika kwa mujibu wa malengo yaliyokusudiwa.

114. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Programu imepangiwa kutumia **Sh. 6,259,900,000** kwa matumizi ya mishahara na mengineyo. **(Kiambatanisho nam. 2).**

### *3.3.11 Fungu E07: Programu ya Usimamizi wa Utumishi wa Umma*

115. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuendelea kupitia na kupitisha Miundo ya Taasisi na Miundo ya Utumishi itakayowasilishwa Kamisheni;
ii. Kuimarisha ukusanyaji wa taarifa katika Utumishi wa Umma pamoja na kuangalia utekelezaji wa Miongozo mbalimbali iliyotolewa na Kamisheni;
iii. Kufanya Ukaguzi wa kawaida katika Taasisi za Umma 72, Ukaguzi maalum katika taasisi 20 Unguja na Pemba;
iv. Kupokea na kuzitolea maamuzi rufaa na malalamiko kutoka kwa watumishi na mamlaka za nidhamu; na
v. Kuandaa Ripoti ya Hali ya Utumishi wa Umma 2023/2024.

**116.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Programu imepangiwa kutumia **Sh. 1,735,900,000** kwa matumizi ya kawaida. **(Kiambatisho Nam. 2).**

### *3.3.12 Fungu E08: Programu ya Usimamizi wa Uajiri, Haki na Nidhamu kwa Watumishi Serikalini*

**117.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-
i. Kusimamia uajiri 4,470 kwa kuzingatia sifa na vigezo vinavyostahiki;
ii. Kusimamia haki na nidhamu za watumishi wa Serikali ikiwa ni pamoja na kupokea na kusikiliza malalamiko ya watumishi wasioridhika na uamuzi unaotolewa na Mamlaka za Nidhamu zilizo chini ya usimamizi wa Tume;
iii. Kuratibu uidhinishwaji wa ajira za mkataba 22, kuthibitisha kazi watumishi 2,820, kubadilisha kada watumishi 194, kupandisha daraja watumishi 862, kutoa nyongeza za muda wa utumishi 18, likizo bila ya malipo 11 na kustaafisha kisheria watumishi wa Serikali 821;
iv. Kutoa mafunzo ya uelewa kwa watumishi na waombaji ajira 1,467, kuimarisha huduma za kiutawala na za

kiuendeshaji na kuwapatia mafunzo ya muda mrefu watumishi watatu (3) na muda mfupi watumishi (2) wa Tume ya Utumishi Serikalini ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

**118.** **Mheshimiwa Spika,** Programu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, imepangiwa kutumiya **Sh. 1,305,800,000** kwa matumizi ya kawaida. **(Kiambatisho Nam. 2).**

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 SHUKRANI NA HITIMISHO

### 4.1 Shukrani

119. **Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, natoa shukurani zangu za dhati kwa washirika wa maendeleo na taasisi zote za ndani zilizoshirikiana nasi kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2023/2024 katika kutekeleza majukumu yetu. Naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru na kuwataja wachache ambao ni:- Jamhuri ya Watu wa China, Korea ya Kusini, India, Saudia Arabia, Oman, Ireland, Malaysia, Switzerland, Uingereza. Mashirika ya Kimataifa ni pamoja na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa (UNDP), Jumuiya ya Kimataifa ya Wanawake (UN Women), Kituo cha Watoa Huduma za Kisheria (Legal Service Facility), Benki ya Dunia (World Bank), Benki ya Maendeleo ya Kiislamu (IDB), Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU), 'BASEL Institute' na Jumuiya ya Kiafrika ya Uongozi na Utawala wa Umma (AAPAM).

120. **Mheshimiwa Spika,** shukurani zangu maalum ziwaendee viongozi wenzangu katika Wizara na nikianza Ndugu. Mansura Mosi Kassim, Katibu Mkuu, Ndugu. Omar Haji Gora, Naibu Katibu Mkuu (Utumishi na Utawala Bora), Ndugu. Mzee Ali Haji Naibu Katibu Mkuu (Katiba na Sheria), Afisa Mdhamini, Wakurugenzi wa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora. Aidha, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mtendaji Mkuu wa Mahkama na Warajis, Waheshimiwa Majaji na Mahakimu wote, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu na Naibu wake, Mkurugenzi wa Mashtaka na Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Naibu wake, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka

ya Kuzuwia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi, Mufti Mkuu na Kadhi Mkuu na Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Serikali Mtandao kwa kuendelea kutekeleza majukumu yao vizuri ya kusimamia utoaji wa haki na huduma kwa wananchi.

121. **Mheshimiwa Spika,** nawashukuru, Wenyeviti wa Tume na Kamisheni, Makamishna na Wajumbe wote waliomo katika taasisi hizi, Wakuu wa Vitengo na Divisheni pamoja na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora na taasisi zake kwa kuendelea kujituma kwa juhudi na maarifa katika kutekeleza malengo na majukumu ya Ofisi yetu. Niwaombe tuendelee kushirikiana katika utekelezaji wa majukumu yetu ya kila siku na kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora kwa wananchi na utoaji wa haki kwa wakati.

122. **Mheshimiwa Spika,** vilevile, nawashukuru Taasisi zote za Kiraia zinazoshirikiana na Wizara yangu, watoa Msaada wa Kisheria wote tunawapongeza kwa mashirikiano yao na moyo wao wa kujitolea. Watambue kwamba jitihada zao zina mchango mkubwa katika upatikanaji wa haki na Serikali inathamini juhudi zao.

123. **Mheshimiwa Spika,** natoa shukrani za pekee kwa Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi mbalimbali za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kushirikiana nasi kwa karibu katika kutekeleza majukumu yetu. Juhudi zetu za pamoja ni muhimu katika kudumisha Muungano wetu.

124. **Mheshimiwa Spika,** kipekee nawashukuru wahusika wote wa Sekta ya Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambao wametupatia ushirikiano wa kutosha katika kuendeleza Sekta hii. Shukrani zangu za pekee nazitoa kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na wafanyakazi wote kwa kuchapa vizuri hotuba hii.

## 4.2 Hitimisho

125. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora itaendelea kusimamia na kutekeleza majukumu yake yote muhimu katika uendeshaji wa nchi yetu, kuimarisha utawala bora na upatikanaji wa haki kwa wakati ili kuhakikisha kuwa Sekta ya Sheria, Utumishi na Utawala Bora inaendelea kutoa mchango mkubwa katika ukuaji wa demokrasia na uchumi wa nchi yetu.

126. **Mheshimiwa Spika,** kwa madhumuni ya kuiwezesha Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kutekeleza majukumu yake na malengo yalioelezwa katika hotuba hii, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Sh. Bilioni 121,778,058,820.** Kati ya fedha hizo, **Sh. Bilioni 42,726,300,000** zitatumika kwa ajili ya mishahara, **Sh. 24,157,100,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo **Sh. 87,000,000** ruzuku ya matumizi mengineyo kutoka Serikalini na **Sh. 57,516,858,784** ni ruzuku kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na Miradi ya Maendeleo.

127. **Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa hoja.

**MWAL. HAROUN ALI SULEIMAN (MBM)**
**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora**
**ZANZIBAR**

**Kiambatisho Nam 1a: Makusanyo ya Mapato Julai/Machi 2023/2024 na Makadirio ya Mwaka 2024/2025**

| | **Makusanyo Julai/ Machi 2023/2024** | | | **Makadirio Mwaka 2024/2025** |
|---|---|---|---|---|
| **IDARA/TAASISI** | **Makadirio** | **Makusanyo** | **%** | |
| Mahkama | 1,576,000,000 | 341,047,498 | **22** | 1,239,900,000 |
| **Jumla** | **1,576,000,000** | **341,047,498** | | **1,239,900,000** |
| Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali | 325,000,000 | 73,000,000 | **22** | 322,400,000 |
| **Jumla** | **325,000,000** | **73,000,000** | | **322,400,000** |
| Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana | 220,000,000 | 127,919,573 | **58** | 272,800,000 |
| **Jumla** | **220,000,000** | **127,919,573** | | **272,800,000** |
| Chuo Cha Utawala wa Umma | 2,035,900,000 | 1,439,564,558 | **71** | 3,243,805,000 |
| **Jumla** | **2,035,900,000** | **1,439,564,558** | | **3,243,805,000** |
| Skuli ya Sheria | 379,000,000 | 51,940,000 | **14** | 179,500,000 |
| **Jumla** | **379,000,000** | **51,940,000** | | **179,500,000** |
| **Kituo cha Sheria** | | 243,309,729 | | |
| | | **243,309,729** | | **334,060,000** |
| **Jumla Kuu** | **4,535,900,000** | **2,033,471,629** | **45** | **5,258,405,000** |

**Kiambatisho Namb 1b:Muhtasari wa Upatikanaji wa fedha 2023/2024(katika,000)**

| | MAKADIRIO KWA MWAKA 2023/2024 | | | | | FEDHA ZILIZOPATIKANA KWA MWAKA 2023/2024 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **PROGRAMU KUU/PROGRAMU NDOGO** | **MISHAHARA** | **MATUMIZI MENGINEYO** | **JUMLA YA FEDHA ZILIZOKADIRIWA** | **MISHAHARA** | **%** | **MATUMIZI MENGINEYO** | **%** | **JUMLA YA FEDHA ZILIZOPATIKANA** | **%** |
| **Programu ya masuala ya kisheria** | | | | | | | | | |
| Usimamizi wa masuala ya kisheria | 108,333,200 | 115,000,000 | **223,333,200** | 108,976,115 | **101** | 49,411,130 | **43** | **158,387,245** | **71** |
| **Jumla ya programu** | **108,333,200** | **115,000,000** | **223,333,200** | **108,976,115** | | **49,411,130** | | **158,387,245** | **71** |
| **Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora** | | | | | | | | | |
| Usimamizi wa Utawala Bora | 216,566,320 | 100,000,000 | **316,566,320** | 111,455,215 | 51 | 42,212,785 | 42 | **153,668,000** | **49** |
| **Jumla ya Programu** | **216,566,320** | **100,000,000** | **316,566,320** | **111,455,215** | | **42,212,785** | | **153,668,000** | **49** |
| **Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa ORKSUUB** | | | | | | | | | |
| Uendeshaji na Utawala | 1,645,301,480 | 1,100,000,000 | **2,745,301,480** | 1,542,536,939 | 94 | 742,487,777 | 67 | **2,285,024,716** | 83 |
| Mipango, Sera na Utafiti | 189,462,960 | 150,000,000 | **339,462,960** | 170,356,953 | 90 | 75,026,314 | 50 | **245,383,267** | 72 |
| Uratibu wa ORKSUUB-Pemba | 336,024,020 | 174,000,000 | **510,024,020** | 250,567,480 | 75 | 76,000,000 | 44 | **326,567,480** | 64 |
| **Jumla ya Programu** | **2,170,788,460** | **1,424,000,000** | **3,594,788,460** | **1,963,461,372** | | **893,514,091** | | **2,856,975,463** | **79** |
| **Programu ya Uendelezaji wa Utumishi wa Umma** | | | | | | | | | |
| Mipango na Maendeleo ya Watumishi | 335,667,400 | 300,000,000 | **635,667,400** | 322,194,008 | 96 | 77,689,848 | 26 | **399,883,856** | 63 |
| Miundo na Mifumo ya Taasisi | 519,344,620 | 193,700,000 | **713,044,620** | 452,565,169 | 87 | 101,172,147 | 52 | **553,737,316** | 78 |
| **Jumla ya Programu** | **855,012,020** | **493,700,000** | **1,348,712,020** | **774,759,177** | | **178,861,995** | | **953,621,172** | **71** |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jumla ya Programu-G01** | **3,350,700,000** | **2,132,700,000** | **5,483,400,000** | **2,958,651,879** | | **1,164,000,001** | | **4,122,651,880** | **75** |
| **Ruzuku G01** | | | | | | | | | |
| Chuo Cha Utawala wa Umma | 2,386,900,000 | | **2,386,900,000** | 1,979,777,839 | 83 | | | **1,979,777,839** | 83 |
| Skuli ya Sheria | | 370,600,000 | **370,600,000** | | | 260,497,000 | 70 | **260,497,000** | 70 |
| **Jumla ya Ruzuku -G01** | **2,386,900,000** | **370,600,000** | **2,757,500,000** | **1,979,777,839** | 83 | **260,497,000** | 70 | **2,240,274,839** | 81 |
| **JUMLA KUU-G01** | **5,737,600,000** | **2,503,300,000** | **8,240,900,000** | **4,938,429,718** | | **1,424,497,001** | | **6,362,926,719** | **77** |
| | | | | | | | | | |
| **Programu ya Usimamizi wa Upatikanaji wa Haki** | | | | | | | | | |
| Usimamizi wa Upatikanaji wa Haki | 7,462,900,000 | 3,767,600,000 | **11,230,500,000** | 4,990,241,014 | 67 | 1,454,102,388 | 39 | **6,444,343,402** | 57 |
| Ruzuku ya Mahkama ya Kadhi | 1,461,800,000 | 219,200,000 | **1,681,000,000** | 979,633,081 | 67 | 137,619,000 | 63 | **1,117,252,081** | 66 |
| **JUMLA KUU-G02** | **8,924,700,000** | **3,986,800,000** | **12,911,500,000** | **5,969,874,095** | | **1,591,721,388** | | **7,561,595,483** | **59** |
| **Programu ya Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Sheria Serikalini** | | | | | | | | | |
| Usimamizi wa Utekelezaji wa Kesi za Jinai | 2,379,400,000 | 988,800,000 | 3,368,200,000 | 1,928,682,507 | 81 | 465,721,520 | 47 | 2,394,404,027 | 71 |
| **JUMLA KUU-G03** | **2,379,400,000** | **988,800,000** | **3,368,200,000** | **1,928,682,507** | | **465,721,520** | | **2,394,404,027** | **71** |
| **Programu ya Usimamizi wa Utekelezaji wa Kesi za Jinai** | | | | | | | | | |
| Usimamizi wa Utekelezaji wa Kesi za Jinai | 2,621,300,000 | 1,000,400,000 | 3,621,700,000 | 2,248,125,843 | 86 | 378,656,000 | 38 | 2,626,781,843 | 73 |
| Ruzuku ya Kituo cha Sheria | | 158,700,000 | 158,700,000 | | | 45,225,000 | 28 | 45,225,000 | |
| **JUMLA KUU - GO4** | **2,621,300,000** | **1,159,100,000** | **3,780,400,000** | **2,248,125,843** | | **423,881,000** | | **2,672,006,843** | **71** |
| **Programu ya Usimamizi wa Mapitio ya Sheria** | | | | | | | | | |
| Usimamizi wa | 827,400,000 | 1,039,300,000 | 1,866,700,000 | 628,951,598 | 76 | 334,905,619 | 32 | 963,857,217 | 52 |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mapitio ya Sheria | | | | | | | | | |
| **JUMLA KUU - G05** | **827,400,000** | **1,039,300,000** | **1,866,700,000** | **628,951,598** | | **334,905,619** | | **963,857,217** | **52** |
| **Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini** | | | | | | | | | |
| Uendeshaji na Usimamizi wa Wakfu, Hijja na Zakka | 1,347,600,000 | 582,500,000 | 1,930,100,000 | 1,077,597,464 | 80 | 229,419,306 | 39 | 1,307,016,770 | 68 |
| **JUMLA KUU - G12** | **1,347,600,000** | **582,500,000** | **1,930,100,000** | **1,077,597,464** | | **229,419,306** | | **1,307,016,770** | **68** |
| **Programu ya Huduma za Serikali Mtandao** | | | | | | | | | |
| Huduma za Serikali Mtandao | 1,249,700,000 | 1,958,900,000 | 3,208,600,000 | 1,097,650,589 | 88 | 550,300,000 | 28 | 1,647,950,589 | 51 |
| **JUMLA KUU - G13** | **1,249,700,000** | **1,958,900,000** | **3,208,600,000** | **1,097,650,589** | | **550,300,000** | | **1,647,950,589** | **51** |
| **Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini** | | | | | | | | | |
| Usimamizi na Uratibu wa Taasisi wa Taasisi na Masuala ya Kiisalmu | 1,347,600,000 | 582,500,000 | 1,930,100,000 | 824,336,107 | 61 | 198,000,000 | 34 | 1,022,336,107 | 53 |
| **JUMLA KUU - G14** | **1,347,600,000** | **582,500,000** | **1,930,100,000** | **824,336,107** | | **198,000,000** | | **1,022,336,107** | **53** |
| **Programu ya Usimamizi ya Maadili ya Viongozi wa Umma** | | | | | | | | | |
| Usimamizi wa Maadili ya Viongozi wa Umma | 640,800,000 | 660,300,000 | 1,301,100,000 | 710,191,936 | 111 | 351,713,250 | 53 | 1,061,905,186 | 82 |
| **JUMLA KUU - G15** | **640,800,000** | **660,300,000** | **1,301,100,000** | **710,191,936** | | **351,713,250** | | **1,061,905,186** | **82** |
| **Programu ya Ukaguzi na Udhibiti wa Rasilimali za Umma** | | | | | | | | | |
| Ukaguzi na Udhibiti wa Rasilimali za Umma | 4,483,900,000 | 1,808,500,000 | 6,292,400,000 | 5,250,822,012 | 118 | 1,190,297,650 | 66 | 5,063,763,892 | 80 |
| **JUMLA KUU -** | **4,483,900,000** | **1,808,500,000** | **6,292,400,000** | **5,250,822,012** | | **1,190,297,65** | | **6,441,119,662** | **80** |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **E04** | | | | | | **0** | | | |
| **Programu ya Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi** | | | | | | | | | |
| Uzuiji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi | 3,136,200,000 | 1,158,400,000 | 4,294,600,000 | 3,302,835,173 | 105 | 625,000,000 | 54 | 3,927,835,173 | 91 |
| **JUMLA KUU - E05** | **3,136,200,000** | **1,158,400,000** | **4,294,600,000** | **3,302,835,173** | | **625,000,000** | | **3,927,835,173** | **91** |
| **Programu ya Usimamizi wa Watumishi wa Umma** | | | | | | | | | |
| Usimamizi wa Watumishi wa Umma | 728,000,000 | 520,900,000 | 1,248,900,000 | 713,562,249 | 98 | 170,392,000 | 33 | 883,954,249 | 71 |
| **JUMLA KUU - E07** | **728,000,000** | **520,900,000** | **1,248,900,000** | **713,562,249** | | **170,392,000** | | **883,954,249** | **71** |
| **Programu ya Usimamizi wa Uajiri, Haki na Nidhamu kwa Watumishi Serikalini** | | | | | | | | | |
| Usimamizi wa Watumishi wa Umma | 458,600,000 | 409,100,000 | 867,700,000 | 441,357,124 | 96 | 133,111,000 | 33 | 574,468,124 | 66 |
| **Jumla ya Programu - E08** | **458,600,000** | **409,100,000** | **867,700,000** | **441,357,124** | | **133,111,000** | | **574,468,124** | **66** |
| **JUMLA KUU** | **33,882,800,000** | **17,358,400,000** | **51,241,200,000** | **27,746,659,047** | | **8,218,791,615** | | **36,821,376,149** | **72** |

**Kiambatisho namba 1c: Upatikanaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa kipindi cha Julai/ Machi 2023/2024 Na Makadirio kwa Mwaka 2024/2024**

| JINA LA MRADI | MAPITIO 2023/2024 | | | MUELEKEO 2024/2025 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **MCHANGO WA SERIKALI** | **MCHANGO WA WAHISANI** | **JUMLA FEDHA ZILOPATIKANA** | **MCHANGO WA SERIKALI** | **MCHANGO WA WAHISANI** | **JUMLA FEDHA ZILIZOPANGWA KUTUMIKA** |
| Mradi wa Uwezeshaji na Upatikanaji wa Haki Kisheria (LEAP II) | | 969,631,552 | **508,105,500** | | 1,166,858,784 | **1,166,858,784** |
| Programu ya Mageuzi ya Utumishi wa Umma (ZPSRP) | 750,000,000 | | **208,792,850** | 1,000,000,000 | | **1,000,000,000** |
| Programu ya Mageuzi ya Sekta ya Sheria | 250,000,000 | | | 500,000,000 | | **500,000,000** |
| Mradi wa Utoaji wa haki kwa Kuzingatia Jinsia ili kuwasaidia wanawake kukabiliana na Kesi za Ukatili Zanzibar | | 373,600,000 | **235,081,451** | | 350,000,000 | **350,000,000** |
| Mradi wa Ujenzi wa Mahkama za Mikoa na Wilaya | 25,000,000,000 | | **9,081,930,031** | 25,500,000,000 | 28,500,000,000 | **54,000,000,000** |
| Mradi wa Mfumo wa Kieletroniki wa Usimamizi wa Taarifa za Mashauri | 2,000,000,000 | | **0** | 500,000,000 | | **500,000,000** |
| **JUMLA KUU** | **28,000,000,000** | | **10,033,909,832** | **27,500,000,000** | **30,016,858,784** | **57,516,858,784** |

**Kiambatisho nambari 2:Makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025**

| PROGRAMU | MISHAHARA | MATUMIZI YA JUMLA | JUMLA | RUZUKU OC | KAZI ZA MAENDELEO SMZ | KAZI ZA MAENDELEO WAHISANI | JUMLA KUU |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Programu ya msuala ya kisheria** | | | | | | | |
| Usimamaizi wa masuala ya Kisheria | 202,791,520 | 120,000,000 | 322,791,520 | | | | |
| **Jumla Programu** | **202,791,520** | **120,000,000** | **322,791,520** | | | | |
| **Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora** | | | | | | | |
| Usimamzi wa Utawala Bora | 184,168,720 | 119,200,000 | 303,368,720 | | | | |
| **Jumla Programu** | **184,168,720** | **119,200,000** | **303,368,720** | | | | |
| **Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa ORKSUUB** | | | | | | | |
| Uendeshaji na Utawala | 1,838,050,196 | 1,550,000,000 | 3,388,050,196 | | | | |
| Mipango, Sera na Utafiti | 250,376,480 | 150,000,000 | 400,376,480 | | 1,500,000,000 | 1,516,858,784 | 3,016,858,784 |
| Uratibu wa ORKSUUB-Pemba | 445,072,800 | 180,000,000 | 625,072,800 | | | | |
| **Jumla Programu** | **2,533,499,476** | **1,880,000,000** | **4,413,499,476** | | **1,500,000,000** | **1,516,858,784** | |
| **Programu ya Uendelezaji wa Utumishi wa umma** | | | | | | | |
| Mipango na Maendeleo ya Watumishi | 451,471,120 | 390,000,000 | | | | | |
| Miundo na Mifumo ya Taasisi | 648,569,200 | 200,000,000 | | | | | |
| **Jumla Programu** | **1,100,040,320** | **590,000,000** | **1,690,040,320** | | | | |
| **Ruzuku G01** | | | | | | | |
| Chuo Cha Utawala wa Umma | 3,191,100,000 | | 3,191,100,000 | | | | |
| Skuli ya Sheria | 565,500,000 | 444,700,000 | 1,010,200,000 | | | | |
| **Jumla Ruzuku G01** | **3,756,600,000** | **444,700,000** | **4,201,300,000** | | | | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **JUMLA KUU GO1** | **7,777,100,036** | **3,153,900,000** | **10,931,000,036** | | **1,516,858,784** | | **12,447,858,820** |
| **Programu ya Usimamizi wa Upatikanaji wa Haki** | | | | | | | |
| Usimamizi wa Upatikanaji wa Haki | 7,849,900,000 | 4,586,100,000 | 12,436,000,000 | | 26,000,000,000 | 28,500,000,000 | 54,500,000,000 |
| Ruzuku ya Mahkama ya Kadhi | 1,485,600,000 | 479,100,000 | 1,964,700,000 | | | | |
| **JUMLA KUU-G02** | **9,335,500,000** | **5,065,200,000** | **14,400,700,000** | | **26,000,000,000** | **28,500,000,000** | **68,900,700,000** |
| **Programu ya Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Serikali** | | | | | | | |
| Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Serikali | 3,543,100,000 | 2,369,000,000 | 5,912,100,000 | | | | |
| **JUMLA KUU-G03** | **3,543,100,000** | **2,369,000,000** | **5,912,100,000** | | | | **5,912,100,000** |
| **Programu ya Usimamizi wa Utekelezaji wa Kesi za Jinai** | | | | | | | |
| Usimamizi wa Utekelezaji wa Kesi za Jinai | 4,345,100,000 | 1,100,500,000 | 5,446,200,000 | | | | |
| Ruzuku ya Kituo cha Sheria | | 190,400,000 | 190,400,000 | | | | |
| **JUMLA KUU-G04** | **4,345,100,000** | **1,290,900,000** | **5,636,600,000** | | | | **5,636,600,000** |
| **Programu ya Haki na Uwezeshaji Kishariah** | | | | | | | |
| Usimamizi wa Haki na Uwezeshaji Kishariah | 1,530,600,000 | 698,900,000 | 2,229,500,000 | | | | |
| **JUMAL KUU-G12** | **1,530,600,000** | **698,900,000** | **2,229,500,000** | | | | **2,229,500,000** |
| **Programu ya Huduma za Serikali Mtandao** | | | | | | | |
| Huduma za Serikali Mtandao | 1,541,000,000 | 2,154,800,000 | 3,695,800,000 | | | | |
| **JUMLA KUU-G13** | **1,541,000,000** | **2,154,800,000** | **3,695,800,000** | | | | **3,695,800,000** |
| **Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini** | | | | | | | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Usimamizi na Uratibu wa Taasisi na Masuala ya Kiislamu | 1,311,600,000 | 983,700,000 | 2,295,300,000 | 87,000,000 | | | |
| **JUMLA KUU-G14** | **1,311,600,000** | **983,700,000** | **2,295,300,000** | **87,000,000** | | | **2,382,300,000** |
| **Programu ya Usimamizi ya Maadili ya Viongozi wa Umma** | | | | | | | |
| Usimamizi wa Maadili ya Viongozi wa Umma | 1,115,900,000 | 832,400,000 | 1,948,300,000 | | | | |
| **JUMLA KUU-G15** | **1,115,900,000** | **832,400,000** | **1,948,300,000** | | | | **1,948,300,000** |
| **Programu ya Ukaguzi na Udhibiti wa Rasilimali za Umma** | | | | | | | |
| Ukaguzi na Udhibiti wa Rasilimali za Umma | 5,578,600,000 | 2,244,700,000 | 7,823,300,000 | | | | |
| **JUMLA KUU-E04** | **5,578,600,000** | **2,244,700,000** | **7,823,300,000** | | | | **7,823,300,000** |
| **Programu ya Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi** | | | | | | | |
| Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi | 4,928,300,000 | 1,331,600,000 | **6,259,900,000** | | | | |
| **JUMLA KUU-E05** | **4,928,300,000** | **1,331,600,000** | **6,259,900,000** | | | | **6,259,900,000** |
| **Programu ya Usimamizi wa Watumishi wa Umma** | | | | | | | |
| Usimamizi wa Watumishi wa Umma | 1,013,000,000 | 722,900,000 | 1,735,900,000 | | | | |
| **JUMLA KUU-E07** | **1,013,000,000** | **722,900,000** | **1,735,900,000** | | | | **1,735,900,000** |
| **Programu ya Usimamizi wa Watumishi Serikalini** | | | | | | | |
| Usimamizi wa Watumishi wa Umma | 705,900,000 | 599,900,000 | **1,305,800,000** | | | | |
| **JUMLA KU - E08** | **705,900,000** | **599,900,000** | **1,305,800,000** | | | | **1,305,800,000** |
| **JUMLA KUU** | **42,726,300,036** | **24,157,100,000** | **64,174,200,036** | **87,000,000** | **27,500,000,000** | **30,016,858,784** | **121,778,058,820** |

| Kiambatisho Nam 3: Hali ya Mashauri hadi kufikia Mwezi wa Machi 2024 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Aina ya Mashauri** | **Yaliyopokelewa na Kusajiliwa** | **Yaliyotolewa Maamuzi** | **%** | **Yanayoendelea** |
| Jinai | 1,478 | 623 | 42 | 855 |
| Madai | 840 | 247 | 29 | 593 |
| Udhalilishaji | 205 | 142 | 69 | 63 |
| Mahkama ya Kadhi | 1,817 | 1,119 | 62 | 698 |
| Dawa za Kulevya | 73 | 33 | 45 | 40 |
| Mahkama ya Watoto | 45 | 31 | 69 | 14 |
| **JUMLA** | **4,458** | **2,195** | **49** | **2,263** |

| **Kiambatisho Nam 4: Ripoti za Mapitio ya Sheria** | |
|---|---|
| 1 | Ripoti ya Mapitio ya Sheria ya Viapo vya Utii na Barua za Uteuzi Nam 1 ya Mwaka 1986. |
| 2 | Ripoti ya Mapitio ya Sheria ya Utalii Nam 6 Mwaka 2009. |
| 3 | Ripoti ya Mapitio ya Sheria ya Viapo Nam 7 ya Mwaka 1917. |
| 4 | Ripoti ya Mapitio ya Sheria ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Nam 9 ya Mwaka 2007. |
| 5 | Ripoti ya Mapitio Sheria ya Msaada wa Kisheria Nam 13 ya Mwaka 2018. |
| 6 | Ripoti ya Mapitio ya Sheria ya Tume ya Utangazaji Zanzibar Nam. 7 ya Mwaka 1997. |
| 7 | Ripoti ya Mapitio ya Sheria ya Ufilisi sura ya 20 ya Mwaka 1917. |
| 8 | Ripoti ya Mapitio ya Sheria ya Kulinda Utamaduni wa Taifa Nam 1 ya Mwaka 1973. |
| 9 | Ripoti ya Mapitio ya Sheria ya Ukomo ya madai sura ya 12 ya Mwaka 1917. |
| 10 | Ripoti ya Mapitio ya Sheria ya Mirathi (watu wasiokuwa waiislam) sura ya 21 ya Mwaka 1917. |
| 11 | Ripoti ya Mapitio ya Sheria ya Hospitali Binafsi na |
| 12 | Ripoti ya Mapitio Sheria ya Mkataba ya sura ya 149. |

| **Kiambatisho Nam. 5a: WATUMISHI WALIOAJIRIWA KUANZIA JULAI, 2023 HADI KUFIKIA MACHI, 2024** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NO.** | **WIZARA / TAASISI** | **WANAWAKE** | **WANAUME** | **JUMLA** |
| 1 | Wizara ya Afya | 270 | 48 | 318 |
| 2 | Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali | 515 | 176 | 691 |
| 3 | Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi | 1 | 2 | 3 |
| 4 | Wizara ya Fedha na Mipango | 4 | 4 | 8 |
| 5 | Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi | 18 | 23 | 41 |
| 6 | Wakala wa Majengo | 5 | 6 | 11 |
| 7 | Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais | - | 5 | 5 |
| 8 | Wizara ya Habari Utamaduni na Michezo | 1 | 2 | 3 |
| 9 | Wizara ya Katiba Sheria Utumishi na Utawala Bora | - | 1 | 1 |
| 10 | Ofisi ya Rais Ikulu | 1 | 8 | 9 |
| 11 | Jeshi la Kujenga Uchumi | 1 | - | 1 |
| 12 | Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana | - | 1 | 1 |
| 13 | Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka | - | 3 | 3 |
| 14 | Taasisi ya Elimu | 1 | 1 | 2 |
| 15 | Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa | 1 | - | 1 |
| 16 | Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale | 4 | 7 | 11 |
| 17 | Wizara ya Ujenzi na Mawasiliano na Uchukuzi | 1 | - | 1 |
| 18 | Wizara ya Uchumi wa Buluu | 3 | 4 | 7 |
| 19 | Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais | - | 2 | 2 |
| 20 | Wizara ya Biashara na Viwanda | - | 2 | 2 |
| 21 | Wizara ya Maji Nishati na Madini | - | 1 | 1 |
| 22 | Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu | 2 | 4 | 6 |
| **JUMLA** | | **657** | **300** | **957** |

**Kiambatisho Nam. 5b:KAZI ZA TUME YA UTUMISHI SERIKALINI KUANZIA JULAI, 2023 HADI KUFIKIA MACHI, 2024**

| WIZARA/TAASISI | KUTHIBITISHWA KAZINI | NYONGEZA YA MUDA WA UTUMISHI | UAJIRI WA MKATABA | KUSTAAFU KWA MARADHI | KUSTAAFU KWA LAZIMA | KUSTAAFU KWA HIARI | LIKIZO BILA YA MALIPO | KUBADILISHWA KADA | KUACHA KAZI | KUFUKUZWA KAZI | KUPANDISHWA DARAJA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali | 1,523 | 1 | 19 | 2 | 249 | 5 | - | 34 | 1 | 3 | 156 |
| Wizara ya Fedha na Mipango | 5 | - | - | - | - | - | 1 | 25 | - | - | 2 |
| Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo | 5 | - | - | - | - | - | - | 12 | - | - | - |
| Wizara ya Afya | 138 | - | 2 | - | 136 | 4 | - | 78 | 2 | - | 33 |
| Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora | - | - | - | - | 2 | - | - | 3 | - | 1 | 1 |
| Ofisi ya Baraza la Mapinduzi | - | 2 | - | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Wizara Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi | 221 | - | - | 1 | 55 | 1 | - | 25 | - | - | 9 |
| Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Ikulu na Mwenyekiti wa BLM | - | 2 | 2 | - | 1 | - | - | 3 | - | - | 1 |
| Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais | - | - | - | - | 4 | - | - | 2 | - | - | 3 |
| Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais | 2 | - | - | - | 4 | - | - | 5 | - | 1 | 3 |
| Kamisheni ya Utalii | 6 | - | - | - | - | - | - | - | - | - | 1 |
| Baraza la Mji Kaskazini A | - | - | - | - | - | - | - | 3 | - | - | 1 |
| Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji | - | - | - | - | 3 | - | 1 | 2 | - | - | 1 |
| Taasisi ya Nyaraka | 2 | - | - | - | - | - | - | 2 | - | - | - |
| Wizara ya Biashara na Maendeleo | - | - | - | - | 1 | - | - | 4 | - | - | - |
| Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani | - | - | - | - | 1 | - | - | 1 | - | - | - |
| Taasisi ya Kilimo | - | - | - | - | - | - | - | 1 | - | - | - |
| Taasisi ya Utafiti wa Mifugo | 3 | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Wakala wa Majengo | 1 | - | - | - | 3 | - | - | 2 | - | - | - |
| Baraza la Manispaa Kaskazini A | 15 | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Baraza la Mitihani | 5 | - | - | - | - | - | - | 1 | - | - | - |
| Baraza la Manispaa Magh.B | - | - | - | - | - | - | - | 2 | - | - | 1 |
| Baraza la Manispaa Mjini | - | - | - | 4 | - | - | - | 3 | 1 | 2 | - |
| Bodi ya Huduma za Maktaba | - | - | - | - | - | - | - | 1 | - | - | 5 |
| Mamlaka ya Kuzuia rushwa na uhujumu uchumi | - | - | - | - | - | - | - | 7 | - | - | 4 |
| Afisi ya Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa | - | - | - | - | 2 | - | - | - | - | - | 1 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Kusini | - | - | - | - | - | - | - | 2 | - | - | 1 |
| Kamisheni ya Ardhi | 9 | - | - | - | 4 | - | - | 1 | - | - | 1 |

| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi | - | - | - | - | 2 | - | - | 4 | - | - | - |
| Baraza la Manispaa Magh. A | - | - | - | - | - | - | - | 2 | - | - | - |
| Ofisi ya Mwanasheria Mkuu | 9 | - | - | - | - | - | - | - | - | 2 | 24 |
| Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja | - | - | - | - | - | - | - | 2 | - | - | 4 |
| Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja | - | - | - | - | - | - | - | 2 | - | - | 1 |
| OR Kazi Uchumi na Uwekezaji | - | - | - | - | 1 | - | - | 7 | - | - | 2 |
| Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba | 10 | - | - | - | 1 | - | - | 5 | - | - | 1 |
| Tume ya Uchaguzi | - | - | - | - | 3 | - | - | - | - | - | 2 |
| Baraza la Mji Kati | - | - | - | - | - | - | - | 6 | - | - | 2 |
| Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | - | - | - | - | - | - | - | 11 | - | - | - |
| Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi | 13 | - | - | - | - | - | - | 4 | - | - | 1 |
| Mamlaka ya Hifadhi ya Mji Mkongwe | - | - | - | - | - | - | - | 2 | - | - | - |
| Chuo cha Kiislamu | 2 | - | - | - | 1 | - | - | 1 | - | - | - |
| Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi | 9 | - | - | 1 | - | - | - | - | - | - | 3 |
| Halmashauri ya Wilaya Micheweni | - | - | - | - | - | - | - | 2 | - | - | - |
| Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar | 4 | - | - | - | 5 | - | - | 1 | - | - | - |
| Mamlaka ya Madawa ya Kulevya | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | 1 |
| Hospitali ya Rufaa Mnazi Mmoja | - | - | - | - | - | - | - | 20 | 1 | - | 7 |
| Ofisi ya mkurugenzi wa Mashtaka | - | - | - | - | 4 | - | - | - | - | - | - |
| Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana | - | - | - | 1 | - | - | - | - | - | - | - |
| Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale | - | - | - | - | 7 | - | - | 6 | - | - | 2 |
| Wizara ya Maji Nishati na Madini | 10 | - | - | - | - | - | - | 2 | - | - | - |
| Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ | - | - | 2 | - | - | 1 | - | 3 | - | - | - |
| Wizara ya Maendeleo ya Jamii | 4 | - | - | - | 1 | - | - | 5 | - | - | 1 |
| Baraza la Mji Mkoani | - | - | - | - | - | - | - | 2 | - | - | 1 |
| Wakala wa Vipimo | 1 | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Tume ya Utumishi Serikalini | 1 | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Tume ya Kurekebisha Sheria | - | - | - | - | 2 | 1 | - | 1 | - | - | 1 |
| Baraza la Mji Chake Chake | 45 | - | - | - | - | - | - | 6 | - | - | 3 |
| Wakala wa Serikalini Mtandao | 4 | - | - | - | - | - | - | 2 | - | - | - |
| Ofisi ya Ufuatiliaji na Usimamizi wa Utendaji Serikalini | - | - | - | - | 1 | - | - | - | - | - | - |
| Tume ya Mipango | - | - | - | - | 1 | - | 1 | - | - | - | - |
| Wakala wa Barabara | - | - | - | - | - | - | - | 1 | - | - | - |
| Baraza la Mji Wete | - | - | - | - | - | - | - | 3 | - | - | - |
| **JUMLA KUU** | **2,057** | **5** | **25** | **8** | **557** | **12** | **3** | **330** | **5** | **9** | **280** |

**Kiambatisho Nam 5c: MALALAMIKO YA WAFANYAKAZI KWA KIPINDI CHA JULAI- MACHI 2023/2024**

| NAM | WIZARA/TAASISI | IDADI YA WATUMISHI | AINA YA LALAMIKO LILOWASILISHWA | UAMUZI ULIOFIKIWA NA TUME |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Wizara ya Afya | 1 | Kuhusiana na Ajira | Dai limekubaliwa na muhusika ametakiwa kusubiri nafasi za kazi zitoke ili aombe tena |
| 2 | Wizara ya Afya | 1 | Kupatiwa haki zake za mshahara na posho | Dai linaendelea kushughulikiwa |
| 3 | Baraza la mji Chakechake | 1 | Kuhusiana na haki za kustaafu kazi | Dai linaendelea kushughulikiwa |
| 4 | Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali | 1 | Utoro kazini | Dai limeshughulikiwa na muhusika ameachishwa kazi kwa mujibu wa kifungu cha 8 cha mkataba wa ajira |
| 5 | Wizara ya Habari Utamaduni na Michezo | 1 | Kupinga kustaafu kazi kwa lazima | Dai linaendelea kushughulikiwa |
| 6 | Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali | 1 | Kusimamishwa kazi kwa kosa la kutohudhuria kazini | Dai linaendelea kushughulikiwa |
| 7 | Mamlaka ya Maji Chakechake | 1 | Kulipwa mafao | Dai limeshughulikiwa kwa muhusika kutakiwa kuwasilisha ombi lake sehemu husika |
| 8 | ZAPSWU | 1 | Kulipwa baada ya kukaimu kwa muda mrefu | Dai limeshughulikiwa kwa muhusika kutakiwa kuwasilisha ombi lake sehemu husika |
| 9 | Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) | 1 | Kulazimishwa matumizi ya Mshahara wake | Dai limeshughulikiwa kwa muhusika kutakiwa kuwasilisha ombi lake sehemu husika |
| 10 | Wizara ya Kilimo | 1 | Marekebisho ya Haki | Dai linaendelea kushughulikiwa |
| 11 | Wizara ya Habari | 1 | Kupinga Taarifa ya Kustaafu | Dai Limekataliwa |
| 12 | Wizara ya Afya | 1 | Kukataliwa Likizo Bila Malipo | Dai Limekataliwa |
| | **Jumla** | **13** | | |